# BRICS

## (Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini)



# Mkakati Mbadala wa Ushirikiano wa Kimaendeleo?



Imeandaliwa na Darlene K. Mutalemwa na Deo P. Mutalemwa

Kuchapwa 2014

Kwa Maswali au Maelezo zaidi Wasiliana na:

Policy Forum

S.L.P 38486

Dar es Salaam

Namba za Simu: +255 22 2780200 / +255 782 317434

Tovuti: www.policyforum.or.tz

Barua pepe: info@policyforum.or.tz

ISBN: 978-9987-708-11-6

© Policy Forum

Hitimisho na maoni yaliyotolewa katika taarifa hii na uchambuzi uliotolewa katika tathmini hii sio lazima uwe mtizamo wa Policy Forum. Kila jitihada zimefanyika ili kuthibitisha usahihi wa habari zilizomo katika tathmini hii, ikiwa ni pamoja na madai yote.

Hata hivyo, Policy Forum haiwezi kuthibitisha usahihi na ukamilifu wa yaliyomo. Ingawa sehemu yoyote ya mapitio haya inaweza kutolewa tena ilimradi chanzo chake kinukuliwe kikamilifu, Policy Forum haitakubali kuwajibika kwa matokeo ya matumizi kwa sababu nyingine au katika muktadha tofauti.

Kimesanifiwa na Kupigwa Chapa na: Jamana Printers Limited
P.O Box 5584
Dar es Salaam, Tanzania

# YALIYOMO

MUHTASARI: JE, UBIA WA TANZANIA NA BRICS: NI MKAKATI MBADALA WA USHIRIKIANO WA KIMAENDELEO? ..............3

1.0 UTANGULIZI ........................................................4

2.0 MSAADA ..............................................................7

CHINA ............................................................10

INDIA..............................................................15

BRAZIL............................................................16

AFRIKA KUSINI..................................................16

URUSI .............................................................17

3.0 BIASHARA.........................................................17

4.0 UWEKEZAJI .......................................................23

5.0 UHAMIAJI .........................................................27

6.0 MATOKEO YA UTAFITI NA MAUDHUI YAKE................29

7.0 HITIMISHO .......................................................32

# MUHTASARI

## Je, Ubia wa Tanzania na BUICAK (BRICS): ni Mkakati Mbadala wa Ushirikiano wa Kimaendeleo[1]?

Mandhari ya hali halisi ya ushirikiano wa kimaendeleo inabadilika huku kukiwa na ongezeko la washirika wapya ambao ni Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini, unaojulikana kwa pamoja kama BRICS . Washirika hawa wapya ambao wanawakilisha fursa mpya, rasilimali mpya na makubaliano mapya ya mikataba; huku mkazo mkubwa zaidi ukilenga katika mwelekeo thabiti wa ukuaji wa kiuchumi, kupunguza umaskini na kupata maendeleo ndivyo vinavyoleta changamoto kwa mashirika ya kimaendeleo na wajasiriamali wa nchi za magharibi.

Utafiti huu, ambao unatokana na kusoma vitabu pamoja na nyaraka mbali mbali za kitaalam, unachangia katika uchambuzi wa maslahi ya sasa ya BRICS kwa Tanzania kwa upande mmoja, (na maslahi ya Tanzania-kwa nchi hizi-kwa upande mwingine), kwa kutoa mtazamo wa kuongeza maarifa na ufahamu wa nafasi ya BRICS na, faida na athari zake kwa Tanzania, nchi ya Afrika Mashariki yenye kipato cha chini. Utafiti huu unalenga katika kutoa majibu stahiki kwa maswali yafuatayo: Je, ni mambo gani yanayozihamasisha hizi nchi (BRICS) kufanya ubia na Tanzania? Je, baadhi ya hizi nchi za BRICS ni wabia wanaofaa zaidi (kwa Tanzania) kuliko wengine? Je, kukua kwa ushirikiano kati ya Tanzania na BRICS katika nyanja za misaada, biashara, uwekezaji na uhamaji ndiyo suluhisho endelevu katika kuchangia maendeleo ya Tanzania? Ili kujibu maswali haya, tunahitajika kuangalia kwa kina juu ya yale ambayo BRICS inayafanya katika uhalisia wake.

Matokeo yanayoshtusha zaidi yaliyojitokeza kutokana na utafiti huu ni kwamba, ubia wa BRICS na Tanzania umegubikwa na mambo mazuri mengi na madhaifu mengi vile vile ikiwa ni pamoja na (japo si hayo tu) yafuatayo: (i) kila nchi iliyo ndani ya huu ubia inashirikiana na Tanzania kwa njia tofauti kabisa kutokana na tofauti katika fikra, maslahi, vipaumbele na mahusiano tofauti ya kihistoria. Hali hii inaashiria kwamba itachukua muda mrefu kabla ya kufikia msingi unaowaunganisha pamoja. (ii) BRICS ni wabia muhimu wa maendeleo, wawekezaji na wabia wa kibiashara, vile vile ni vyanzo muhimu vya wasambazaji wa miradi kwa Tanzania. Tanzania ni nchi ambayo inahifadhi jumuiya mbali mbali za nchi wanachama wa BRICS. Hali kadhalika, Tanzania inategemea BRICS kama chanzo cha hazina lukuki zenye mfano wa kuigwa (iii) kwa namna nyingi, wimbi la hivi karibuni la kuja kwa nchi hizi (BRICS) nchini Tanzania, huku wakiwa

[1] Maoni, matokeo ya utafiti, takwimu, tafsiri na masharti yaliyotolewa katika utafiti huu ni ya watafiti, hivyo hayawakilishi maoni ya Policy Forum  Tunapokea kwa shukurani maoni ya Semkae Kilonzo, Chambi Chachage na Nicholas Lekule.

wamekuja na mijadala na uzoefu uliojikita kwenye ujuzi wao wa kimaendeleo wa kisasa, umepanua uwanja wa maendeleo na mlango wa kupenya kwa Tanzania umeongezeka. Masharti yale ya zamani yaliyokuwa yanabana hayatumiki tena, na serikali ya Tanzania haihitaji tena kubanwa na sheria/kanuni/(masharti ya) za misaada ya kimaendeleo ya nchi za magharibi. Wafanyabiashara mbalimbali wa nchi hizo wanaweza kupambanishwa wao kwa wao, lakini bado hakuna ubia unaletwa usio na kamba zinazovutia upande mwingine (usio na maslahi yao) pamoja na uwepo wa maneno ya kisiasa ya ushirikiano wa nchi zilizo kusini mwa Afrika ambao unazingatia zaidi manufaa/(kunufaika kwa) ya kila upande/ pande zote mbili  (iv) Kadiri hizi nchi za BRICS zinavyoendelea kuimarisha uhusiano wake na Tanzania, mifumo na uwezo wa kutoa mwongozo, kusimamia, kutathmini na kuwajibika kwa ajili ya shughuli zao havijapewa kipaumbele na uwekezaji  stahiki. Uchambuzi huu unahitimisha kwa kutoa mapendekezo kadhaa kwa lengo la kuwasilisha vipengele ambavyo vitakuwa na manufaa kwa pande zote mbili, kati ya BRICS na Tanzania, kwa kuwa Tanzania inashauku ya kupata maendeleo ya haraka.  Mwisho wa siku, hali hii itategemea zaidi busara na hekima za uongozi wa kitaifa wenye maono na nguvu ya Taasisi za Tanzania katika kushawishi ubia wa BRICS ili uwe kwa ajili ya manufaa ya watanzania. BRICS (kwa maana hiyo nchi nyingine yoyote), haitabadilisha Tanzania: Bali Watanzania ndio watakaoibadilisha Tanzania.

## 1.0 Utangulizi

BRICS ni kifupisho cha kundi la nchi tano kubwa zinazoendelea ambazo ni; Brazil, Urusi, India, China na Afrika kusini[2]. Nchi hizi za BRICS zinatofautishwa kutokana na tabia zao (kidemografia) na uwezo wao wa kiuchumi zikiwa ni kati ya nchi kubwa duniani zenye nguvu sana kiuchumi katika karne ya 21 (na kuwa na nafasi kubwa ya kufikia ukuaji huo) . Ingawa China na India ndizo zinazoongoza kundi hili, pengine kukua kwa nafasi ya China katika Afrika kunaweza kuwa ndiyo mjadala mkubwa kwa jinsi BRICS inavyojihusisha na nchi zinazoendelea. Brazil ni nchi tajiri sana kwa kuwa na rasilimali kama vile kahawa, maharage ya soya, miwa, madini ya chuma, pamoja na mafuta mabichi, huku ikiwa na takriban asilimia 60 ya ardhi inayolimika (ambayo ni asilimia 7 tu ya eneo lote la ardhi

[2] Wazo la kuwa na BRIC [Brazil, Russia, India and China] lilibuniwa kwa mara ya kwanza na Goldman Sachs mnamo  mwaka 2001 kama sehemu ya zoezi la urekebishaji uchumi ili kuwa na maono ya ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha nusu karne ijayo;  jina hili la BRIC  lilitumiwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2001 na Goldman Sachs katika jarida la uchumi la kimataifa namba  66, " Dunia inahitaji Washirika (BRICS) Bora zaidi wa Kiuchumi".Mawaziri wa mambo ya nchi za nje wa  BRIC  katika mkutano wao huko New York tarehe 21 septemba, 2010 walikubaliana kwamba kulikuwa na uwezekano wa  Afrika Kusini kukaribishwa kujiunga na BRIC.     Kwa msingi huo, Afrika Kusini ikawa imekaribishwa kuhudhuria mkutano wa tatu  wa BRIC huko Sanya, China tarehe 14 Aprili, 2011.http://www.bricsindia.in/about.html, [ilitembelewa tarehe 05/02/2013]

yake) lakini ina asilimia 31.2 ya sehemu ya ardhi yote kwa ajili ya kilimo. Urusi ni nchi inayojulikana kwa kuwa na hifadhi ya mafuta mengi sana, gesi asilia, na madini. India ni nchi iliyosheheni hazina kubwa katika kutoa huduma za ushauri wa kitaalam, huku kukiwa na hali ya kuinuka katika viwanda vya utengenezaji bidhaa; Wakati ambapo China imekuwa karakana ya viwanda vya utengenezaji bidhaa duniani ikiwa na nguvukazi yenye utaalam na ujuzi wa hali ya juu pamoja na gharama chini katika malipo ukilinganisha na hali halisi.

Afrika Kusini ndiyo nchi ya 26 miongoni mwa nchi zenye nguvu ya kiuchumi duniani, ikiwa na pato la jumla la uchumi wa ndani (GDP) kiasi cha dola za marekani bilioni 357, na ndiyo lango muhimu la kibiashara na uwekezaji kwa sehemu kubwa ya Afrika. Ni nchi yenye ukubwa wa wastani ikiwa na jumla ya eneo la ardhi ambalo ni zaidi kidogo ya kilomita za mraba 1.2 na takriban asilimia 12 ya ardhi inayofaa kwa kilimo. Hii ndiyo nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa platinamu na kromiamu na imebeba hazina kubwa ya manganizi, makundi ya chuma ya aina ya platinamu, Kromiamu, vanadiamu, na 'alumino-silicates' . Afrika Kusini inazalisha asilimia 45 ya mahitaji yote ya umeme katika Afrika na kampuni ya ufuaji umeme ya 'African power supplier' inatoa umeme ambao ni wa nne kwa kuwa na gharama ya chini katika ulimwengu mzima[3].

Kwa upande wa nafasi ya umadhubuti wa kiuchumi duniani, China ni nchi ya 27 (kati ya nchi 139) mwaka 2010-11, wakati ambapo nafasi ya kiuchumi za nchi nyingine za BRICS ni kama ifuatavyo: India (51), Afrika Kusini (54/139), Brazil (58/139), na Urusi (63/139), kwa mtiririko huo. Kuwa katika nafasi nzuri kwa nchi ya China kunaweza kuwa kumesababishwa na nafasi yake pana katika soko la dunia (2/139), mazingira yake mazuri ya uchumi mpana (4/139), na ugunduzi (26/139). Nafasi ya viashiria mbali mbali vya kuongoza katika ushindani unadhihirisha kwamba BRICS wana masoko ya ndani yaliyo imara na yasiyotikisika[4].

Ingawa nchi za BRICS hazijafikia kiwango cha kuwa na hadhi ya viwanda ambayo huipa sifa ya kuwa wabia wa Kamati ya misaada ya Kimaendeleo na pamoja na kugubikwa na hali ya kutokuwa na usawa na umaskini, wameweza kuongeza misaada ya kifedha na misaada ya kiufundi pia wameanzisha njia na mbinu mbalimbali za ushirikiano wa kiuchumi katika nyanja kadhaa hasa kupitia ushirikiano wa kiuchumi wa nchi za kusini (South-South cooperation) ambao unasisitiza Misingi ya Usawa, Mshikamano na Maendeleo ya pande zote mbili ikiwemo kuinua hali ya nchi zenye kipato cha chini (LICs) kama vile Tanzania. Mikutano mikuu ya ngazi ya kimataifa (HLF) juu ya matumizi stahiki ya misaada

---

3 Serikali ya India-Wizara ya Fedha (2012) Ripoti ya BRICS: Utafiti juu ya Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini ambao ulilenga zaidi juu ya Africa with special focus on synergies and complementarities. Oxford University Press: India

4 kama ilivyo hapo juu

(aid effectiveness) iliyofanyika Paris (2005), Accra (2008), na Monterrey (2002) haikuweza kutambua nafasi ya nchi za BRICS kama nchi zinazoibukia kuwa wabia wa maendeleo (nchi zinazotoa misaada), lakini mkutano wa Busan wa mwaka 2011 wa HLF[5] uliweza kuzitambua nchi za BRICS kama wahamasishaji walio dhahiri kwa ajili ya mabadiliko katika ubunifu wa mpango wa maendeleo duniani[6] (global development architecture)


Wakati wa kuhitimisha mkutano wao uliofanyika kule Durban Machi Mwaka 2013[7], viongozi wa nchi za BRICS walitangaza azma yao ya kuanzisha benki mpya ya maendeleo itakayolenga katika kutafuta na kukusanya rasilimali kwa ajili ya miundombinu na miradi ya maendeleo endelevu katika nchi za BRICS na katika nchi nyingine zinazoinuka kiuchumi na nchi zinazoendelea ili kuunga mkono jitihada zinazofanyika kuzihusisha nchi nyingi zaidi na taasisi za kikanda za fedha kwa ajili ya kuingia ukuaji wa uchumi na maendeleo duniani. Bank hiyo inaweza kuziongezea nguvu taasisi zilizopo na kushughulikia mapungufu na changamoto katika sekta nyeti(kama ilivyoainishwa wakati wa mkutano wa tano wa BRICS mwaka huu, 2013.

5 ubia wa kimataifa kwa ajili ya ushirikiano madhubuti wa kimaendeleo, ulioanzishwa huko Busan, Korea ya Kusini mnamo mwaka 2011, ndio ulioweka viwango vya kimataifa juu ya kanuni za usimamizi mzuri wa misaada na kiwango stahiki cha maendeleo ambavyo wadau wote wa maendeleo wanapaswa kuvizingatia. Kanuni hizi ni pamoja na: uongozi wa nchi na umilikaji wa mikakati ya maendeleo; kuelekeza nguvu zaidi kwa matokeo yanayowanufaisha masikini zaidi katika nchi zinazoendelea; ubia jumuishi miongoni mwa wabia wa maendeleo unaozingatia msingi wa kuwa na imani kila moja na mwenzake; na uwazi na uwajibikaji kila moja na mwenzake. Wadau wote wa maendeleo-wakiwemo wafadhili wa siku zote na wale wanaoibukia-wanapaswa kuheshimu na kuunga mkono kanuni hizi za msingi kwa kutimiza ahadi walizojiwekea huko Busan. Ili lengo hili liweze kutimia, ubia wa maendeleo wa kimataifa unapaswa kuzingatia maono yanayotekelezeka, utashi wa ushirikiano wa kisiasa kutoka ngazi ya juu kabisa pamoja na mfumo bora wa uwajibikaji kimataifa na unaoendena na hali halisi ya kimazingaira.

6 Umoja wa Ulaya ( 2012) Nafasi ya BRICS katika dunia inayoendelea . kurugenzi kuu ya sera kwa ajili ya sera za nje ya umoja wa ulaya: Brussels

7 http://www.brics5.co.za/about-brics/summit-declaration/fifth-summit/

## Jedwali 1.1: kulinganisha viwango vya ukuaji wa kiuchumi, madeni na sifa nyinginezo miongoni mwa nchi za BRICS




**Chanzo :** imetengezwa kutokana na ile ya Swingonski (2012)[8]

## Je, ushirikiano kati ya nchi za BRICS na Tanzania una manufaa gani kwa Tanzania?

Kujiunga kwa Tanzania na nchi za BRICS, kunaashiria kuwepo kwa fursa mpya, rasilimali mpya na makubaliano mapya ya (kuingia mikataba)kufanya kazi na zaidi ya yote ni safari ya kuelekea kwenye ukuaji wa ngazi ya juu kiuchumi, kupunguza umaskini na kupata maendeleo. Halikadhalika, kuongezeka kwa nguvu ya upangaji bei kwa nchi zinazoendelea katika mikataba na biashara za kimataifa kama ilivyodhihirishwa katika mazungumzo ya Shirika la Biashara la Kimataifa yaliyofanyika Doha ambayo yametolewa kama sababu nyingine za kushirikiana na nchi za BRICS.

8 Swingonski F ( 2012) kujenga BRICS ya Misaada ya nje : mwanachama mpya kabisa wa klabu. Kituo cha kuchambua ustawi duniani. Inapatikana http://globalprosperity.wordpress.com/2012/11/12/building-brics-of-foreign-aid-newest-member-of-the-club/, [ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

Kwa kuongezea, ushirikiano wa nchi za kusini mwa Afrika umeundwa kwa namna ambayo unaendana sana na mazingira ya kiafrika, ambao unachangia kwa kiasi kikubwa katika hali ya kukubalika kwake. Kiuhalisia zaidi, ni kwamba umeegemea zaidi katika kanuni ya msingi, ajenda na malengo yake ya maendeleo yanapangwa na nchi za kusini. Haupaswi kuendeshwa kwa njia ya michango ya hiari na mamlaka ama mahusiano tegemezi. Kinyume chake, unadai kuwa unaegemea katika misingi ya usawa, mshikamano, kuheshimu uhuru wa nchi na maamuzi yao wenyewe, kufaidishana (hali ya kukuza mafanikio ya kila moja) na kuwezeshana. Msingi wa kutoingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine, ni wa muhimu, hasa kwa ajili ya kuepukana na kuwapa au kulazimisha utoaji maelekezo ya usimamizi na ya kisera, badala yake, kuheshimu haja ya kuwa na utatuzi wa matatizo unaofanywa na nchi yenyewe husika na kuwapa nafasi ya wao kujipangia sera zinazowafaa. Mkazo mkubwa zaidi umeelekezwa katika ubia na kushirikishana uzoefu, hususan katika nyanja za ushirikiano wa kiufundi na kuhamisha elimu. Umoja wa ushirikiano wa nchi za kusini, mara nyingi umejikita katika miradi, kwa kawaida bila masharti katika mchakato wa usimamizi, sera za kiuchumi au marekebisho. Mara nyingi umekuwa ukihusishwa na gharama ndogo za ubadilishanaji, sambamba na utekelezaji wa haraka zaidi.

Ni kutokana na hoja hizi za kihistoria ndiyo maana utafiti huu umelenga katika kutoa mawazo na kuchunguza zaidi maarifa kuhusu nafasi na matokeo ya BRICS nchini Tanzania, nchi iliyoko Afrika Mashariki na yenye kipato cha chini. Utafiti huu unalenga kuchangia majibu stahiki ya maswali yafuatayo: (i) Je, ni mambo gani yanayohamasisha nchi za BRICS kuingia ubia na Tanzania? (ii) Je, baadhi ya nchi za BRICS ndio washirika wazuri wa biashara (kwa Tanzania) kuliko nchi nyingine? Na (iii) je kuibuka kwa uhusiano wa BRICS na Tanzania katika nyanja za misaada, biashara, uwekezaji na uhamiaji ni suala endelevu katika kuchangia maendeleo ya Tanzania?

Tutachambua kila kipengele cha maeneo hayo ya ushirikiano kwa kina lakini kwa muhtasari hapa chini.

## 2.0 MISAADA

Misaada ya nje imetumika sana katika maendeleo ya nchi za Afrika tangu miaka ya 1960. Nchi nyingi kati ya nchi hizi za Afrika, hususan zilizoko katika kusini mwa Sahara, zimeendelea kutegemea misaada kutoka nje tangu zilipopata uhuru. Tanzania na yenyewe ni mojawapo katika kundi hili.

BRICS ni kundi la washirika wa maendeleo ambalo haliko kwenye Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na Kamati yake ya Misaada ya Maendeleo (DAC). Pamoja na hayo, kundi hili limepata umaarufu na kusababisha hali ya kuwa kivutio ndani ya jumuiya ya maendeleo ya kimataifa. Washirika hawa wa maendeleo wamekuwa wakijulikana kama: ‘wapya’, ‘wanaoibuka’, ‘wasio wa kawaida’, ‘wasio wa magharibi’, auambao hawako katika Kamati ya

Misaada ya Maendeleo (DAC)'. Lakini majina hayo wanayoitwa yanarahisisha tu kundi ambalo ni la tofauti na ngumu kulielewa.

Kukua kiuchumi kwa watoaji wa misaada ya maendeleo, kunaashiria kwamba nchi zinazoendelea kama vile Tanzania zinaweza kushirikiana na washirika wa maendeleo ili kunufaika na fursa. (angalia jedwali 2.1) Hali hii pia husababisha nafasi pana zaidi ya kufanya maamuzi na fedha zaidi, na serikali za nchi zilizoendelea zinafurahia fursa hii. Zaidi ya hapo, ni kwamba, hali hii husaidia kuimarisha nguvu ya kushawishi suala la bei kwa serikali za nchi zinazopokea misaada, na hili linaweza kusababisha ugumu zaidi kwa washirika wa maendeleo kuingilia suala la mwelekeo wa sera katika nchi zinazoendelea.

**Jedwali 2.1: Muhtasari wa Mpangilio wa Ubia kati ya BRICS na Washirika wa kawaida wa Maendeleo nchini Tanzania**

| | Sekta | Utaratibu | Kupitia chombo |
|---|---|---|---|
| **BRICS** | Afya, kilimo, elimu, ulinzi, miundombinu<br>Uwekezaji katika sekta inayozalisha | taratibu zinazoendana na hali ilivyo, uzingativu wa gharama, na uzingativu wa muda muafaka katika utekelezaji haraka wa miradi | Uhusiano baina ya nchi na nchi, msaada unakuwa mikononi mwa mtoaji wakati wa utaratibu wa manunuzi na unatolewa moja kwa moja kwa aliye na mradi (kwa hivyo unakuwa nje ya bajeti) |
| **Washirika wa maendeleo**<br>**Wa kawaida** | Sekta zote zinazotoa kipaumbele sekta za kijamii, malengo ya maendeleo ya Milenia, biashara huria, ukuzaji/ utetezi wa demokrasia na haki za\| binadamu, ustawi na hifadhi ya jamii. | njia za kawaida za msaada wa fedha ikiwa ni pamoja na: mfuko wa fedha za kusaidia bajeti,fedha za miradi, mfuko wa misaada ya pamoja.<br>Kuzingatia umuhimu wa maazimio ya Paris/Accra/ Busan na kuzingatia ajenda zilizopitishwa; huku mkazo mkubwa ukielekezwa katika kujenga uwezo, utawala bora, uwazi, kuhusisha mashirika yasiyo ya serikali na uwajibikaji. | Uchaguzi wa chombo gani kitumike litabainishwa kwa kuangalia vigezo ikiwemo aina ya mbia, mukhtadha, na uimara wa taasisi za fedha za umma.<br>Washirika ni pamoja na taasisiza serikali, mashirika ya kimataifa, asasi zisizo za serikali, ushirikiano kati ya mashirika ya umma na yale ya binafsi, hii ikiwa ni mifano michache tu. |

**chanzo:** waandishi wa chapisho hili (2013)

Falsafa za BRICs kwa ajili ya kusaidia kifedha miradi ya maendeleo zinatofautiana sana na zile za "washirika wa maendeleo wa kawaida" (wanachama wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na Kamati yake ya Misaada ya Maendeleo (OECD-DAC) kwa njia kuu tatu (Mwase na Yang, 2013[9]): (i) Msingi wa utendaji wa BRICS, ukiachilia mbali Urusi, umejengwa juu ya kanuni ya kunufaishana. Sehemu kubwa ya misaada ya fedha inaelekezwa kwenye sekta ya miundombinu ili kuunga mkono shughuli za uzalishaji. Urusi, kama ilivyo kwa wafadhili wa kawaida, hivi karibuni imelenga zaidi katika kuinua hali ya kijamii, kwa kuzingatia kwamba kupunguza umaskini ndiyo lengo kuu la ODA yao;(ii) baadhi ya nchi za BRICs, hasa China, zina kawaida ya kutoa misaada isiyo ya kifedha kwa ajili ya miradi ambayo haiambatani na masharti ya kisera. Wanalichukulia hili kama sehemu ya msingi ya kutoingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine; na kama mbinu ya kuepukana na rushwa. Tofauti yake, ni kwamba, wafadhili wa kawaida wanachukulia masharti ya kisera katika kujengea uwezo taasisi na utawala bora kama ndiyo suala la msingi zaidi katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya misaada; na

(iii) dhana za matumizi endelevu ya madeni zinatofautiana, kwa BRICs kulenga zaidi uendelevu wa ngazi ya miradi midogo midogo wakati ambapo wafadhili (washirika wa maendeleo) wa kawaida wakitilia mkazo zaidi mpango wa muda mrefu kwa nchi husika kufanya matumizi endelevu ya madeni huku ikizingatia masuala ya uchumi mpana.

Kwa kuongezea, ni kwamba, hizi nchi za BRICS hazitilii mkazo masharti ya utawala bora, sera za kiuchumi na utendaji mzuri wa kitaasisi au marekebisho ya kitaasisi katika ushirikiano wao.Vile vile hawatilii mkazo suala la kuoanisha (kusawazisha) na uratibu ili kuboresha matumizi mazuri ya madeni kama ilivyokuwa imeazimiwa katika Azimio la Paris.

Mara kadhaa imeshuhudiwa kwamba juhudi za BRICS katika kufadhili miradi ya maendeleo imesaidia kupunguza tatizo la miundombinu na kupunguza umaskini katika nchi zenye kipato cha chini ingawaje kwa ujumla kumekuwa na ukosefu wa takwimu toshelevu na zinazotolewa kwa wakati kwa nchi za BRICS pamoja na nchi zinazopokea misaada.  Kwa upande mwingine, baadhi ya nchi wanachama zinatoa angalizo kwamba kumekuwa na msisitizo mkubwa zaidi juu ya "miradi ya kijamii" badala ya kujenga uwezo wa uzalishaji na kupunguza umaskini kwa haraka na kwa manufaa ya muda mrefu ujao[10].

9 Mwase N na Yang  Y ( 2012) falsafa za "BRICs' kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo na athari zake kwa LICS"makala zilizofanyiwa tafiti kwa ajili ya matumizi ya  IMF12/74, Shirika la Fedha la Kimataifa

10 kama ilivyo hapo juu

## China

*"Mahusiano ya Kusaidiana kati ya Tanzania na China yametuweka karibu na kuwa kama ndugu.. Watanzania kamwe hawawezi kusahau msaada muhimu na ukarimu wa China katika miongo kadhaa sasa "(Rais Kikwete aliyasema hayo nchini China 2006/06/23 kama yalivyorejewa na Sandvand (2007[11]).*

Katika miaka ya karibuni, China imeongeza misaada yake ya maendeleo nchi za nje kwa nchi zenye kipato cha chini hasa za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Takwimu zilizopo - ambazo ni ushahidi tosha[12]- zinaonesha kwamba kwa mfano misaada ya China imekuwa ikiipita ile ya wafadhili wa siku zote (Financial Times, 2011[13]). Sababu tatu za kawaida zinazoifanya China isichapishe kiwango cha misaada kinachotoa kwa nchi za Afrika, zimetolewa (Davies ameitaja katika Huse na Muyakwa, 2008[14]).

Kwanza, China yenyewe bado ni nchi inayoendelea na hivyo idadi kubwa ya watu wa China wangeweza kupinga kuwasaidia Waafrika badala ya kuwasaidia watu maskini nchini China. Pili, China inahisi kwamba hii inaweza kuwa ni taarifa nyeti kwa nchi zinazopokea misaada yake hivyo ni juu ya nchi za Afrika kuchagua kama wanataka kutoa taarifa kuhusu uwingi wa misaada wanayopokea.Tatu China haitaki mataifa ya Afrika kulinganisha kiasi cha misaada wanachokipokea miongoni mwao. Tunahisi ukweli kwamba China kwa ujumla si jamii iliyo wazi nchini mwake katika suala la kuchapisha kirahisi kile kinachofanywa na serikali, sababu hii pengine ni tabia ambayo imeenda mbali na kuwa sehemu ya mahusiano yake ya misaada na Afrika. Pia kuna wanaodai licha ya kutofautiana na maelezo na wanaoifurahia misaada ya China ambao wanadai kwamba China inataka kuionesha Afrika namna gani misaada yake ilivyo bora ilikinganishwa na ile ya nchi za Magharibi.

11 Andvand, H. (2007): Marafiki na nia na malengo . Ulinganifu wa misaada kutoka China na ile inayotoka Nchi za Scandnavia kuja Tanzania., : Chuo Kikuu cha Sayansi Asilia cha Norway (Norwegian University of Life Science)

12 Kiasi halisi cha misaada ya kimaendeleo kutoka china kuja Tanzania ni vigumu kukithibitisha kwa vile takwimu hazitolewi kati ya nchi na nchi na misaada ya china iko nje ya mfumo wa usimamizi wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na Kamati yake ya Misaada ya Maendeleo (DAC). Hali kadhalika, makubaliano ya misaada kati ya Tanzania na China ni ya siri, kwa maana hiyo, hapaswi kuhojiwa na umma. Ni vema ikaeleweka wazi kwamba kwa kutokuwa na uwazi katika misaada yake, serikali ya china imefungua mlango wa kutuhumiwa na kueleweka vibaya.

13 Kwa mfano, China iliishinda Benki ya Dunia akiwa ameongoza katika kutoa mikopo nchi za nje kwa nchi zinazoendelea kupitia Benki yake ya mandeleo (China Development Bank) na Beniki yake ya Uagizaji na uuzaji bidhaa nje (China-Export-Import Bank) unaofikia kiasi cha dola kimarekani bilioni 110 kati ya mwaka 2009 na 2010

14 Huse, M. D. na Muyakwa, S. L. (2008). Kuwepo kwa china katika Afrika: utoaji mikopo, Nafasi Ya Sera na Utawala Bora (Oslo, Norway ) kampeni ya Norway kwa ajili ya kufuta madeni na Baraza la Norway kwa ajili ya Afrika.

Misaada ya Maendeleo ya nje kutoka China kuja Tanzania hutofautiana kwa kiasi kikubwa na ile ya wafadhili wa kawaida.kwa kuwa hutolewa kama miradi ya misaada, misaada ya kiufundi au aina ya misaada inayotolewa kama ruzuku, mikopo isiyo na riba inayolipwa kwa kipindi cha muda mrefu, au karibuni zaidi, kama mikopo ya riba nafuu. Kwa maoni ya Bräutigam (2007), alitoa mfano katika Huse na Muyakwa (2008[15]), kwamba miradi ya Kichina inajulikana kama 'uthibitisho wa uwezo'. Upendeleo wa mara kwa mara kwa ajili ya mradi wa misaada ni uamuzi wa kimkakati - ni njia ya China kudhihirisha, au tuseme uwepo wake katika nchi. Aidha, inaweza pia kuwa mradi wa misaada huchukuliwa kuwa mfumo sahihi zaidi kwa ajili ya China kuonesha uhodari wake zaidi na nguvu kazi, kwa kutumia teknolojia rahisi na makampuni ya ujenzi yenye ushindani hasa[16]. Misaada ya China pia inatambulisha bidhaa ambazo hazijulikani au bidhaa za Kichina katika masoko ya wapokeaji (Haroz, 2011[17]).

Imedaiwa kwamba misaada ya maendeleo ya nje ya China kwa Tanzania inatolewa katika kukabiliana na mahitaji yaliyooneshwa na Tanzania. Kwa mfano mwaka 2006, Waziri Mkuu wao, Wen Jiabao alisema kuwa; "upande wa China utaelekeza misaada yake kwenye kilimo, umwagiliaji na maendeleo ya miundombinu katika ushirikiano wake wa kiuchumi na kiteknolojia na Tanzania, ili kukidhi mahitaji ya upande wa Tanzania" (Xinhua 2006/06 / 24, alitoa mfano katika Sandvand 2007[18]).

Kwa hakika, misaada ya China imeelekeza upendeleo wake kwenye miradi ya miundombinu (kwa mfano ni pamoja na maeneo magumu kama vile barabara za vijijini, madaraja juu ya makorongo marefu na mito yenye kasi kubwa, na bandari zenye kina-bahari) – ambayo misaada ya wafadhili wa kawaida wa nchi za Magharibi wamekuwa wakisita kufadhili (Lancaster, 2007[19]). Misaada hii inathaminiwa na serikali za Afrika kwa ajili ya kusaidia uchumi kama vile mikoa ya Kusini-Magharibi mwa Tanzania imefunguliwa baada ya kujengwa reli ya TAZARA (kama ilivyoelezwa hapo chini), na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na ufanyaji biashara kuwa wa ushindani zaidi.

15 kama ilivyo hapo juu.

16 Sandvand, H. (2007): marafiki na nia na malengo , ulinganifu wa misaada ya china na misaada ya nchi za scandinavia kwa Tanzania : Chuo Kikuu cha Sayansi Asilia cha Norway

17 Haroz D (2011) China katika Afrika: Ufaano au unyonyaji? The Fletcher Forum of World Affairs, Vol 25:2 Summer

18 Sandvand, H. (2007):marafiki na nia na malengo : Chuo Kikuu cha Sayansi Asilia cha Norway (Norwegian University of Life Science)

19 Lancaster, C ( 2007), Mfumo wa misaada ya kichina, Kituo cha Utafiti wa Maendeleo Duniani (Center for Global Development Essay) , inapatikana http://www.cgdev.org/content/publications/detail/13953, [ilitembelewa tarehe 25/05 2008]

Utoaji wa miundombinu unachukuliwa na Tanzania kwa kiasi kikubwa kuwa ni muhimu sana. Kwa mfano, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA ) unasema: "Katika kutambua haja ya kuboresha matarajio ya kiuchumi ya sekta za uzalishaji na huduma za jamii, kuna haja ya kuboresha upatikanaji wa miundombinu hasa" (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2005: 8[20]).

Hata hivyo, utoaji wa miundombinu ya China sio ya kipekee nchini Tanzania, ikifahamika kuwa misaada ya China inaunga mkono sekta za kilimo, afya na ulinzi kama zilivyo nyinginezo kwa jambo hilo. Hivyo katika mtazamo wa msaada huu wa sekta mbalimbali, inawezekana ikawa sahihi kujiuliza kama ni China peke inaitikia kwa mahitaji ya nchi wapokeaji wa misaada-, au kama wao hutoa msaada wa ndani ya maeneo ambayo wao wana maslahi fulani nao ni washindani. Zaidi ni kwamba, wakati MKUKUTA unabainisha sekta kuu tatu kwa ajili ya uboreshaji - ukuaji wa uchumi (nguzo ya I), uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii (Nguzo ya II), na utawala bora na uwajibikaji (Nguzo ya III), misaada ya China imejikita katika nguzo ya I na II, na hakuna msaada unaotolewa kwa ajili ya utawala bora na uwajibikaji, na Misaada ya pamoja ya kibajeti (GBS) ambao ni mfumo unaopendelewa na serikali ya Tanzania.

GBS ni kweli haitajwi na Wachina. Kama vile, njia ya kukabiliana na mahitaji ya nchi zinazopokea haionekani kama njia sahihi ya misaada ya China kwa Tanzania (Sandverg, 2007).

Moshi na Mtui (2008:13) wamebainisha kwamba Tanzania ni mpokeaji mkubwa wa misaada toka China kwa nchi za Afrika[21] na kwamba haitaonekana fahari kusisitiza kuwa Tanzania imekuwa hailazimishwi kupokea misaada inayopata toka China.

Kwa hivyo si jambo la ajabu inapotokea kwamba Serikali ya China imeweka mkazo kidogo juu ya kuoanisha mambo yanayohusu misaada na jumuiya ya wafadhili ya kimataifa. Ukweli ni kwamba, kuhusiana na Tanzania, hakuna viashiria vya masuala ya misaada ya China kugongana na ile ya wafadhili wengine wa kimataifa na hakuna ahadi ilivyotolewa na uongozi wa China wa kuandaa misaada yao na nchi mpokeaji kwa mifumo ya usimamizi wa fedha. China si mwanachama wa OECD -DAC au Kikundi cha Washirika wa Maendeleo au PDG (sawa DAC katika Tanzania).

[20] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2005) Mkakati wa kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (1).Ofisi ya Makamu wa Rais: Dar-Es-Salaam

[21] Moshi H na Mtui J ( 2008) uchambuzi makini juu ya mahusiano ya kiuchumi kati ya Afrika na China (Scoping studies on Africa-China Economic Relations): Kisa Mafunzo cha Tanzania, ripoti iliyopitiwa upya na kukabidhiwa AERC, Nairobi (A Revised report submitted to AERC, Nairobi)

Wao hawajatia saini makubaliano ya pamoja kati ya serikali ya Tanzania na wadau wa maendeleo chini ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada kwa Tanzania (JAST), na wala hawashiriki katika mikutano ya mashauriano na wafadhili wala kushiriki sehemu yoyote katika mchakato wa JAST. Wakati China imeridhia Azimio la Paris (na kwa hivyo iliahidi kushirikiana na wafadhili wengine kuoanisha misaada yake), imekuwa ikidaiwa kwamba China pengine ilifanya hivyo kwa nafasi yake kama mpokeaji msaada, zaidi kuliko kama mfadhili (Sandberg, 2007 ).

China imekuwa na ushirikiano katika masuala ya misaada na Afrika tangu miaka ya 1950 na 1960, wakati China ilipoanzisha miradi ya kilimo na afya, na kujenga viwanda katika nchi mpya za Afrika zilizokuwa zimejikomboa kutoka katika makucha ya kikoloni.

Kwa mfano, mwaka 1965 China ilikubali kufadhili na kujenga kiwanda cha zana za kilimo chaUbungo Farm Implements (UFI) nchini Tanzania. Awali kikiwa na uwezo wa kuzalishaji tani 1,000 za zana za kilimo, kupanua hadi tani 2,000 mwaka 1980, wakati huo kiwanda kilitosheleza asilimia 85 ya mahitaji ya zana za mkono nchini (Yu, 1975 alirejea kwenye Sandvand, 2007). Miaka michache baadaye, mnamo mwaka 1970, nchi hizi mbili zilikubaliana kuhusu ujenzi wa shamba la kitaifa la Mbarali. Shamba hilo lilikamilika mwaka 1977, likiwa na ukubwa wa ekari 8,000 za ardhi, duka la kukarabati vifaa vya kilimo , kinu cha kukoboa na kusindika mchele- kikiwa na uwezo wa tani 8,000-10,000 kwa mwaka za mchele, shamba la kuku wapatao 50,000 na shamba la ng'ombe wa maziwa 100. 'Mafanikio ya kushangaza' yalipatikana katika kipindi cha miaka 1978 -1984, na gharama za uwekezaji zikalipwa katika kipindi cha miaka sita tu (Ping 1999: 177 alirejea kwenye Sandberg 2007).

Hata hivyo, Hutchinson (1975) katika mfano wake wa Sandvand (2007) anadai kuwa, sababu nyingine iliifanya Tanzania kuipokea kwa mikono miwili misaada ya China katika miaka ya mwanzo ni kutokana na shauku ya Rais Nyerere kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya vijijini - eneo ambalo aliamini misaada ya kiufundi ya China ingekuwa ya thamani kubwa zaidi.

Mfano mwingine ni TAZARA, reli ya Tanzania-Zambia, ambayo yawezekana ni mfano maarufu wa mikopo ya mwanzo kabisa kutoka China. Ilijengwa mwaka 1964 kwa wahandisi 50,000 wa Kichina na wafanyakazi wenye ujuzi na ikagharimu dola zipatazo milioni 500[22], ulikuwa ndio mradi mkubwa zaidi wa misaada ya kigeni uliotekelezwa na China wakati huo. Mradi huo ulihusu ujenzi wa reli umbali wa kilometa 2000, kuunganisha nchi ya Zambia ambayo haina bandari huku ikipinga ubaguzi wa rangi kutoka ukanda wa shaba, kaskazini mwa

22 Hiki kilikuwa ni kiasi kikubwa kwa china, ambayo ilikuwa nchi maskini sana kuliko nchi nyingi za Afrika katika miaka ya 1970 (Schiere na wenzake (2011)

Zambia na bandari ya Dar-es-Salaam (Brautigam 2008[23]). Nyerere na Kaunda, wakati huo wakiwa marais wa Tanzania na Zambia wote waliisifia sana reli hiyo ya Tanzania-Zambia , wakidai ni "mchango mkubwa kwa watu wa Afrika" na kuusifu kama "Barabara ya Uhuru" na " Mfano bora wa ushirikiano wa nchi za Kusini "(Jamhuri ya Watu wa China, 2000[24]).

Mradi mwingine ulikuwa ni ule wa ujenzi wa Uwanja wa Taifa wa michezo Tanzania wenye uwezo wa kubeba watu 60, 0000 ambao ulikamilika katika robo ya mwisho ya mwaka 2007. Ulijengwa kwa gharama ya jumla ya dola $ 43,500,000, huku asilimia 53 ya gharama ilifadhiliwa na Serikali ya Tanzania na asilimia 47 (US $ 20,500,000) ikiwa ni kwa njia ya mkopo wenye masharti nafuu kutoka China (Moshi na Mtui, 2008). Jambo la kuvutia ni kwamba uhusiano wa China -Tanzania unaimarishwa kwa ziara za mara kwa mara za viongozi wa ngazi ya juu wa China na Tanzania, na kukumbushana mara kwa mara kuhusu urafiki wa China na Tanzania kwa kuashiria manufaa ya pande zote mbili.

Kwa mfano, wakati wa ziara yake ya Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam mwaka 2006, Waziri Mkuu wa China alitangaza:

"Ni vyema uwanja wa Taifa wa Tanzania kuwa ukumbusho wa urafiki na kuimarisha ushirikiano kama ilivyo kwa Reli ya Tanzania-Zambia. Basi ukawe manufaa kwa watu wa Tanzania na kutoa mchango mkubwa wa urafiki kati ya China na Tanzania "(China 2006/06/24 ilirejewa katika Sandvandg, 2007).

Katika suala la huduma za jamii, tangu mwaka 1968, China mara kwa mara imekuwa ikitoa timu ya matabibu kutoka Jimbo la Shandong kwa Tanzania. Takriban wafanyakazi 1,000 wa afya walileta nchini mwaka 2009. Wafanyakazi wa afya wa China mara nyingi huchangia maarifa yao ya kitaalamu kwa kuwafundisha wafanyakazi wa afya wa Tanzania kuhusu namna dawa za Kichina zinavyofanya kazi (Janson na wenzake, 2009[25]).

Hivi karibuni, misaada ya China imekuwa ikihusishwa zaidi na sekta ya maliasili. Kama mtumiaji mkubwa duniani wa chuma, China imekuwa ikishiriki kikamilifu katika utafutaji wa vyanzo muhimu kwenye nchi ambazo inaweza kuanzisha nayo ushirikiano katika uchimbaji wa makaa ya mawe, chuma na uvumbuzi wa gesi.

---

[23] Brautigam, D (2008) misaada ya china kwa Afrika: changamoto ng'ambo ya Atlantic, Mfululizo wa makala za GMF ; yanapatikana http://www.gmfus.org/doc/Brautigam0410aFINAL.pdf, [ ilitembelewa tarehe 25/05/2008]

[24] http://www.fmprc.gov.cn/eng/ziliao/3602/3604/t18009.htm [ilitembelewa tarehe 02/02/2013]

[25] Jansson J,Burke C,Hon T( 2009) Mpangilio wa uwekezaji, Misaada na Biashara wa China katika nchi ya Tanzania, Kituo cha uchambuzi wa masuala suyo China: Chuo Kikuu cha Stellenbosch

Mradi wa pamoja ulioanza mwaka 2012 kati ya China (Sichuan Hongda Co Ltd ambayo ulipokea fedha kutoka katika mabenki ya China) na Tanzania (Shirika la Maendeleo la Taifa -NDC) unahusisha ujenzi wa mgodi wa chuma wa Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Makaa hayo ya mawe yanatarajia kuchangia megawati 600-(MW) katika kituo cha nishati (thermal power station). Wakati huo huo, makubaliano ya mkopo wa dola za marekani bilioni moja ($1 billion loan agreement ) (kutoka China na Benki ya Exim imepangwa kwa ajili ya kujenga bomba kubwa la gesi asilia (urefu wa Kilometa 532 ) kutoka Lango la Mnazi (Mnazi bay) na Songosongo kisiwa cha kusini mwa Tanzania na mji mkuu wa kibiashara wa nchi hiyo, Dar es Salaam ( gazeti la International Business Times, 2011[26]).

Baadhi ya wachambuzi wametoa maoni yao kwamba China inatoa misaada ya kigeni kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika bila masharti ya kisera ambayo inaendana na misaada ya nchi za Magharibi kuhusu uwajibikaji mzuri wa haki za binadamu, usimamizi huria wa uchumi wa nguvu ya soko huria, uwajibikaji wa sera za mazingira na uwazi wa kisiasa kwa upande wa serikali zinazopokea misaada, ambavyo ndivyo vigezo vya utawala bora (Tjønneland et al, 2006).

Sera ya misaada "Bila masharti-" ya China ilizungumzwa sana hivi karibuni katika Mkutano wa Tano wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano wa China –Afrika Julai 2012 uliofanyika Peking,China. Kwa upande mwingine, sera ya China kuhusu kutoingiliwa imekosolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) na wafadhili wa kawaida kwa sababu ya athari zake hasi kwa maendeleo ya kiuchumi na mafanikio katika utawala (Tjønneland et al, 2006).

## India

Kwa upande wa India, takwimu halisi za misaada ya India kwa Tanzania pia ni vigumu kuzipata kwa kuwa India haina utaratibu wa kuripoti taarifa ya misaada yake na mtiririko wake kwa OECD- DAC. Hata hivyo, Tanzania imekuwa moja ya nchi mpokeaji mkubwa wa misaada ya India Maendeleo kwa misaada ya nchi za Nje kati ya nchi mbili (ODA) mbali na Kusini-mashariki mwa bara la Asia[27].

26 Gazeti la The International Business Times (2011) China, Tanzania zimejipanga kushirikiana katika biashara ya makaa ya mawe, chuma, kwa dola za marekani billioni tatu inapatikana: http://au.ibtimes.com/articles/218660/20110923/china-enters-3-billion-coal-iron-deal-with-tanzania.htm [ilitembelewa tarehe 17/05/2012]

27 Bijoy C R ( n.d) India: hali ya mpito kuelekea kuwa mfadhili wa dunia, ripoti maalum ya ushirikiano wa nchi za kusini 2010, inapatikana: http://www.realityofaid.org/userfiles/roareports/roareport_3ce2522270.pdf, ilitembelewa tarehe 20 Disemba, 2011

Misaada ya nchi za nje ya India ni mchanganyiko wa mradi wa misaada, ruzuku ya manunuzi, mikopo, gharama za usafiri, na gharama za mafunzo ya kiufundi inayotolewa na serikali ya India na imeelekezwa hadi kwenye ulinzi[28].

Aidha, miradi bora ya kiufundi[29] imebainika kuwa katika mfumo wa uanzishwaji wake mwaka 1973 na kuendelea kupewa msaada kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo vidogo nchini (SIDO) na Small Industries Corporation (NSIC) ya India. Tanzania pia imekuwa mmoja wa wanufaika wakubwa sana wa mpango ITEC / SCAAP[30] tangu mwaka 1966. Ilianza na wanafunzi 24 kila mwaka, idadi ambayo ikawa inaongezeka hatua kwa hatua hadi 120 kwa mwaka mnamo 2009, na idadi ya wanafunzi sasa ni zaidi ya 1200. Tanzania ni walengwa wakubwa wa ufadhili wa kielimu wa India na misaada mingine ya kielimu ikiwemo ufadhili binafsi katika vyuo vya elimu ya juu vya India. Takriban wanafunzi 5,000 wa Tanzania wanakadiriwa kuwepo nchini India kwa ufadhili binafsi. Vile vile, kuna miradi miwili inayofadhiliwa na serikali ya India, ambayo ni: kituo cha ubora katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) na C-DAC- (a Centre of Excellence in ICT by C-DAC; na the Pan-African e-network project by TCIL[31]).

Mikopo kwa serikali ya Tanzania imekuwa inatolewa na serikali ya India chini ya mkataba uliosainiwa tarehe 5 Juni, 2009 kwa thamani ya dola za kimarekani milioni 40 ili kugharimia sekta ya kilimo[32]. Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Pinda, alizindua awamu ya kwanza ya mradi wa matrekta 288 mnamo Oktoba 2010, ikiwa ni sehemu ya jumla ya matrekta 1860. Hii ililenga kuisaidia serikali ya Tanzania kufanikisha KILIMO KWANZA iliyokuwa imetangazwa sana, kama jitihada ya makusudi kwa ajili ya kufufua sekta ya kilimo na kufanikisha mapinduzi ya kijani nchini Tanzania, ambayo dhana yake imeazimwa kutokana na uzoefu wa India.

Waziri Mkuu wa India, Manmohan Singh, katika ziara yake ya siku tatu kutembelea Tanzania Mei 2011, alizindua misaada kadhaa kwa ajili ya taifa. Hii ni pamoja na mikopo yenye thamani ya $ 191,000,000 , na dola $ 180,000,000 kwa ajili ya miradi ya maji nchini Tanzania, na dola za Marekani 10 milioni kwa ajili ya miradi ya kuzijengea uwezo sekta za kijamii na kielimu na dola milioni moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo. India na Tanzania pia zimesaini makubaliano

28 Gazeti la Daily News la tarehe 3 oktoba, 2012 kuhusu kusambazwa kwa magari kwa wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

29 www.mea.gov.in/meaxpsite/foreignrelation/tanzania.pdf, [ilitembelewa tarehe 12/11/2011]

30 mea.gov.in/mystart.php: ITEC/SCAAP Inaashiria ushirikiano wa kitaalamu katika uchumi (ITEC) na mpango maalum wa msaada wa commonwealth kwa Afrika [ilitembelewa tarehe12/11/2011]

31 Kama ilivyo hapo juu

32 Machapisho ya ubalozi wa India.

ya kuepusha utozaji kodi mara mbili ili kuongeza uwezo zaidi katika uwekezaji na pia mkataba wa kukuza viwanda vidogo vidogo (Chaudhury, 2011[33]).

## Brazil

Brazil inasita kutoa misaada ya kifedha moja kwa moja kwa nchi za Afrika, badala yake inapendelea kutoa misaada ya kiufundi, miradi ya ushirikiano, mafunzo, dhamana, na vyombo vingine kusaidia nchi husika kama vile washirika binafsi wa Brazil na wa umma ( Benki ya Dunia na Taasisi ya Utafiti wa Uchumi ya Brazil , 2011[34]). Tanzania imepokea msaada wa kiufundi katika maeneo yafuatayo: mafunzo na kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wa afya, msaada wa baada ya mavuno ya korosho na kilimo cha bustani, maendeleo ya ufugaji wa samaki na mapambano dhidi ya VVU / UKIMWI[35].

Serikali ya Brazil nchini Tanzania ingependa kutoa msaada mkubwa zaidi katika kusaidia makampuni binafsi ya Brazil yenye nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa soya, miwa, mahindi na pamba, ikizingatia kwa kiasi kikubwa utaalamu wao katika bidhaa hizi za kilimo. Kwa namna hii, wameonesha dhamira ya kushiriki katika Mkakati wa Ukuzaji Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT[36]).

## Afrika Kusini

Msaada wa maendeleo wa Afrika Kusini ulianza kipindi cha ubaguzi wa rangi, ambao ulitumiwa na serikali ya kibaguzi kupata marafiki kati ya nchi za Afrika. Baada ya kwisha kwa ubaguzi wa rangi, serikali mpya ilijihusisha na sera ya mambo ya nje ya "kuhuishwa upya kwa Afrika " ili kujenga mahusiano yenye nguvu zaidi na wengine waliosalia katika bara la Afrika.

Hali hii ilisababisha utaratibu mpya mwaka 2001 wa kuanzishwa kwa Mfuko wa kusaidia harakati za kuzaliwa upya kwa Afrika na Ushirikiano wa Kimataifa Duniani (ARF) ambao ulitoa misaada na mikopo kwa nchi nyingine za Afrika.

---

33 Chaudhury D (2011) uimarishaji wa uhusiano : India imetoa mamilioni lakini bado inataka zaidi. Inapatikana katika http://indiatoday.intoday.in/story/india-offers-millions-but-tanzania-wants-more-grants/1/139601.html [iitembelewa tarehe 02/02/2013]

34 Benki ya Dunia na Taasisi ya utafiti wa kuchumi ya Brazil (2011) kujaza mapungufu ya Atlantic: Brazil na Nchi za Afrika zilizo kusini mwa jangwa la sahara, ushirikiano wa nchi za kusini wakishirikiana kwa ajili ya ukuaji wa kiuchumi Benki ya Dunia: Washington

35 kama ilivyo hapo juu

36 SAGCOT ni Mpango wa uwekezaji katika kilimo unaoendelezwa kupitia sekta binafsi ambo unapata msaada kutoka serikalini. Mpango huu unahusisha mikoa kadhaa ya kusini na kusini magharibi ya Tanzania. Lengo lake ni kuwavutia wawekezaji wakubwa ili waanzishe mashamba makubwa ya kilimo yayakayoleta mabadiliko makubwa ya uzalishajj katika kilimo na wakati huo huo waweze kuwasaidia wakulima wadogo kadiri inavyowezekana.

Huku wakikabiliwa na kuongezeka kwa mahitaji zaidi ya utoaji wa misaada ya nje pamoja na udhaifu katika usimamizi wa Mfuko huo (ARF), mnamo mwaka 2011 serikali ya Afrika Kusini ilianzisha Wakala Mkuu wa usimamizi wa Ubia wa maendeleo ya Afrika Kusini iliyoitwa the South African Development Partnership Agency (SADPA[37])

Afrika Kusini pia inapitisha misaada yake kwa njia ya mipango ya maendeleo inayoshirikisha nchi zaidi ya mbili, kwa mfano kupitia Umoja wa Afrika (AU), SADC, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), au Benki ya Dunia (WB[38]). Hapa vile vile ni vigumu kutoa tarakimu halisi ya uwingi wa misaada inayotolewa na Afrika Kusini. Ingawaje makadirio yanaonesha kwamba matumizi kwa mwaka yanakadiriwa kufikia kati ya Dola za Marekani milioni 100 hadi Dola 400 kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010. Kwa upande wa mpangilio wa uwiano wa usambazaji kijografia, Misaada ya kimaendeleo kutoka Afrika Kusini imelenga zaidi ukanda wa nchi za SADC[39] na kwa mapana zaidi imelenga bara la Afrika[40].

## Urusi

Kama ilivyo kwa wabia wengine wa maendeleo, Urusi nayo haikua wazi kuhusu mtiririko wa misaada yake, vile vile haifuati taratibu na kanuni kadha wa kadha zilizotungwa na nchi za magharibi.

Kwa hivyo wakati ambapo misaada rasmi kutoka Urusi inaweza ikawa midogo kuna ushahidi fulani kwamba nguvu ya wa Urusi katika Afrika unaongezeka. Kama watunga sera kadhaa wa Afrika walivyobainisha, mbinu inayotumiwa na Urusi inafanana na ile ya China-misaada ya maendeleo inaunganishwa kwenye misaada ya biashara, jambo ambalo linaleta ugumu katika kuvitofautisha vema kati ya misaada na biashara. Malighafi ndiyo inayochukua nafasi kubwa, na makampuni ya nchini Urusi yametambua kwamba rasilimali za Afrika yanaweza kusaidia kuongeza nafasi yao katika soko la dunia (Stuenkel, 2012[41]).

---

37 Stahl A K ( 2012) Ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa Washirika watatu: Umoja wa Ulaya, China na Afrika : matarajio yaliyopo kwa Afrika Kusini: Makala ya Uchambuzi. Chuo Kikuu cha Stellenbosh; Afrika Kusini

38 Kama ilivyo hapo juu

39 SADC ni Umoja unaojumuisha nchi zifuatazo:Afrika Kusini, Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) , Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Swaziland, Shelisheli , Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

40 Stahl A K ( 2012)

41 Stuenkel O. (2012) Urusi yaenda Afrika http://www.postwesternworld.com/2012/03/17/russia-goes-to-africa/ [ilitembelewa 01/02/2013]

Urusi imeshafuta madeni yenye thamani ya zaidi ya dola za marekani bilioni 20 yaliyokuwa yametolewa hapo awali kwa nchi za Afrika, hasa hasa kupitia mpango wa "madeni kwa faida ya maendeleo" na kuongeza misaada kwa ajili ya bara hili. Makubaliano ya pamoja na Tanzania ya kubadili madeni na kuwa misaada ya maendeleo yamekwishasainiwa ili kuwatumia madeni kwa minajili ya kufadhili miradi ya maendeleo (Stahl, 2013[42]).

## 3.0 BIASHARA

Mahusiano ya kibishara kati ya China na Tanzania yalianza miaka ya 1964 wakati ambapo China ilianzisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi hii. Makubaliano hayo ya kwanza ya kibiashara kati ya nchi hizi mbili yalitiwa saini mwezi februari mwaka 1965 na kufuatiwa na mingine 1984 (The Barter Trade Protocol), 1985 (Agreement on the Establishment of a Joint Economic and Trade Commission), and 1996 and 1997 (Framework Agreement for the Provision of an Interest-Subsidized Preferential Credit by China to Tanzania) (Sandvand 2007: 97).

Kwa mujibu wa ripoti ya CCS (2006: 51) iliyotolewa katika Sandvand (2007:97), "ukubwa wa biashara umeshuhudia ukuaji wa kushangaza tangu mwaka 1965". Rutaihwa na Mkwawa (2011) wamezidi kufafanua kwamba sera za kiuchumi na soko huria za nchi hizi mbili zimefungua mlango mpana kwa ajili ya ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi ambapo biashara kati ya Tanzania na China imekuwa ikikua kwa kasi kubwa sana tangu mwaka 2004[43].

Jedwali 3.1 linaonesha uuzaji wa bidhaa na uagizaji wake tangu mwaka 2004-2010. Mnamo mwaka 2010, China ilishika nafasi ya kwanza kama mbia wa Tanzania katika biashara akiwa na jumla ya biashara nyingi zaidi kuliko wabia wengine wa biashara. Urari wa faida ya biashara kati ya nchi hizi mbili ulibaki kwa China. China inamiliki takriban asilimia 7.5% ya jumla ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Uagizaji wa bidhaa unaofanywa na Tanzania kutoka China unachukua asilimia takriban 6.0% ya jumla ya bidhaa zinazoagizwa toka nje[44] kwa kutilia mkazo juu ya kukua kwa biashara kati ya China na Tanzania, taasisi za kifedha za Tanzania kama benki za CRDB, Exim, EcoBank hivi karibuni (mwaka 2013) kila mmoja imeanzisha dirisha maalum kwa ajili ya China-idara inayohudumia biashara za kibenki kwa ajili ya wafanyabiashara na wawekezaji wa nchi hizi mbili kwa lengo la kuwawezesha

---

42 http://www.africareview.com/Business---Finance/-/979184/1536944/-/5v6em0/-/index.html [ ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

43 Rutaihwa J and Mkwawa A ( 2011) uchambuzi halisia wa ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara kati ya china na Afrika kwa uzuri au ubaya: uchunguzi kifani wa Tanzania katika jarida la kimataifa la utafiti wa kitaaluma katika biashara na Sayansi za Jamii 2011, toleo la. 1, Na. 3

44 kama ilivyo hapo juu

### Jedwali 3.1: Takwimu ya Biashara kati ya Tanzania na China ( kati ya mwaka 2004 – 2010 katika dola milioni za Marekani)

| Mwaka | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uuzaji wa bidhaa kwenda China | 70.450 | 90.209 | 119.280 | 14.114 | 220.913 | 37.266 | 643.450 |
| Uagizaji wa bidhaa kutoka China | 171.492 | 217.378 | 304.890 | 411.960 | 703.533 | 677.905 | 866.040 |

*Chanzo: Takwimu ya Biashara ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA Trade Statistics (2011) iliyorejewa katika Rutaihwa na Mkwawa (2011:433)*

Katika uuzwaji wa bidhaa zake nje, bidhaa kuu ambazo China inaiuzia Tanzania ni: vyakula, magari, bidhaa za viwandani, mazao ya viwanda vidogo, bidhaa za kemikali, vifaa vya magari, vifaa vya umeme, vifaa vya kieletroniki na chuma cha pua. Kwa upande mwingine, bidhaa kuu ambazo Tanzania inaiuzia China ni vyakula vikavu vya baharini, ngozi mbichi, magogo, shaba ambayo haijasafishwa, vinyago vinavyotokana na miti, pamoja na katani na korosho (Kamndaya, 2010[45]). Vyanzo vingine vya taarifa vinaropoti kwamba China inaagiza kwa wingi madini hasa shaba, na aina ya madini ya thamani ya chuma, na kiasi kidogo cha *(niobium, tantalum, vanadium, zirconium na manganizi),* mboga za majani- na mazao yatokanayo na wanyama kutoka Tanzania (Jansson et al, 2009).

Biashara ya mbao imepewa uzito maalum katika sehemu hii ya uchambuzi kwa sababu kuu mbili:

Kwanza, katika kipindi cha miaka 15 iliyopita China, imetawala biashara yote katika soko la mbao duniani. Mwaka 2009, ilikuwa ndiyo karakana ya mbao iliyokuwa kubwa kuliko zote ulimwenguni, ikiwa inaagiza mita za ukubwa 28,059,700 za magogo– hii ikiwa ni ongezeko la asilimia 177% ikilinganishwa na mwaka 1999. Ongezeko hili katika uagizwaji wa bidhaa toka nje,ni matokeo ya moja kwa moja ya mchanganyiko wa kuongezeka kwa matumizi ya ndani ya nchi, katika nchi ambayo ina rasilimali adimu za misitu, ikiambatana na kuongezeka daima kwa soko kule Marekani, Ulaya na kwingineko kwa ajili ya mazao yatokanayo na magogo ya bei ya chini yanazotengenezwa nchini China. Katika nchi nyingi ambapo China huchukua mbao hizi kumekuwa na usimamizi dhaifu wa misitu.  Kwa sasa, Afrika mashariki inaipatia China asilimia 5.49% tu za mahitaji yake yote ya mbao. Hata hivyo, kwa Tanzania, China ni kituo muhimu

45 Kamndaya S (2010) ,Mtaalam: China ina uchu kwa ajili ya Rasilimali za Afrika , Gazeti laThe Citizen , la tarehe 30 Januari,inapatikana kutoka http://www.thecitizen.co.tz/newe.php?id=17113 [17/05/2012]

mno cha kuuzia bidhaa zetu nje. Mbao zinauzwa kama magogo, jambo ambalo linainyima Tanzania fursa ya kutengeneza mbao ambazo thamani yake ingekuwa kubwa zaidi kutokana na mazao yatokanayo na mbao na ambayo yangeleta manufaa makubwa yakiwemo maisha bora zaidi kwa jamii inayoizinguka misitu (WWF, 2011[46]).

Pili, biashara ya mbao inayoifanya China imegubikwa na uvunaji usioendelevu[47], ukataji haramu wa magogo na ukiukwaji wa haki za jamii zinazoizunguka misitu. Kumekuwa na shinikizo kubwa kutoka kwa jumuiya ya kimataifa na kutoka ndani ya serikali ya China yenyewe kuangalia upya jinsi gani inaweza kuifanya biashara ya mbao kuwa endelevu, ikizingatiwa kwamba kuna mahitaji makubwa ya mbao ambayo bado hawajayakidhi nchini China. Hapa Tanzania peke yake, inakadiriwa kuwa mwaka 2005, kulikuwa na uvunaji haramu wa asilimia 94% ya mbao (kama ilivyorejewa hapo juu) na katika hili, kulikuwa na tuhuma iliyoihusisha China. Moja kati ya takwimu zinazovuta hisia kwa jinsi ya kushangaza katika ripoti iliyotolewa na "TRAFFIC" ambayo ilichapishwa mwaka 2007 iyorekodi viwango vya kutisha vya rushwa, utoroshaji haramu wa magogo na uuzwaji wa mazao yatokanayo na misitu kutoka Tanzania, ilikuwa ni kulinganisha kati ya uuzaji wa halali wa mazao yatokanayo na misitu uliotangazwa na Tanzania kwenda China na ununuzi wa mbao kutoka Tanzania uliokuwa umetangazwa na China. Uchambuzi uliofanyika kwa miaka ya 2003-2005 uligundua kwamba China iliagiza mazao yatokanayo na mbao kutoka Tanzania mara 10 zaidi ya kile kinachoonekana kwenye kumbukumbu ya uuzwaji nje wa mazao hayo, jambo ambalo linamaanisha kuwa Tanzania ilikusanya asilimia 10% tu ya mapato ambayo ilikuwa inastahili.  Hali hii inachangiwa kwa kiasi fulani na uwezo mdogo wa serikali ya Tanzania, serikali za mitaa na serikali kuu katika kutekeleza na kusimamia sheria za misitu. Hili limekuja kuigharimu Tanzania: mwaka 2005, uvunaji haramu wa magogo uliisababishia serikali hasara inayokadiriwa kufikia dola za marekani milioni 58-ambayo ni sawa na gharama ya vyumba vya madarasa ya sekondari 10,000 au usambazaji wa neti za mbu kwa watu milioni 11-ambayo ni robo ya idadi ya watu wote nchini Tanzania[48].

46 WWF (2011) China na Afrika: uwezeshaji wa mazungumzo ya pamoja na kuingia ubia kwa ajii ya Biashara endelevu na uwekezaji, inapatikana : http://assets.wwf.org.uk/downloads/china_africa_poverty_environment.pdf, [ilitembelewa tarehe 17/05/2012]; Milledge, S.A.H., Gelvas, I. K. na Ahrends, A. (2007). Udhibiti wa Misitu na Maendeleo ya Taifa: mambo ya kujifunza kutokana na kuongezeka ghafla kwa magogo kusini mwa Tanzania  TRAFFIC East/Southern Africa /Tanzania Development Partners Group Wizara ya Maliasili na Utalii, Dar es Salaam, Tanzania. [ilitembelewa tarehe  17/05/2012];

47 WWF (2011) China na Afrika: Uwezeshaji wa mazungumzo ya pamoja na kuingia ubia kwa ajili ya Biashara endelevu na uwekezaji, inapatikana http://www.thecitizen.co.tz/newe.php?id=17113(17/05/2012

48 Kama ilivyo hapo juu

Shughuli haramu zinazohusisha ukwepaji kodi hazifanyiki tu katika sekta ya misitu bali pia zinaaminika kuwa zinafanyika katika sekta ya wanyama pori. Ripoti yenye maelezo ya kina iliyoandaliwa na chama cha kulinda tembo dhidi ya ukatili (TEPS) imedhihirisha kwamba pembe nyingi za ndovu zinazouzwa kwa njia ya haramu zinaishia nchini China kutokana na mahitaji makubwa ya pembe za ndovu kule China (Kaijage, 2013[49]).

Kwa upande wa India, bidhaa kuu ambazo Tanzania inaziagiza kutoka India ni pamoja na mafuta ya madini, mafuta, chuma & chuma cha pua, dawa za famasi, magari (pamoja na spea zake), vipande vya chuma & chuma cha pua, mitambo ya umeme, mashine/ vifaa vya umeme, vifaa vya plastiki zikiwemo mifuko milaini (synthetic polymers), vifaa vya mpira yakiwemo matairi n.k., vitu vilivyotengenzwa kutokana na pamba, mavazi & nguo na nafaka. Bidhaa kuu ambazo Tanzania inapeleka India ni pamoja na mboga mboga, kunde, korosho, pamba mbichi, madini ya gemstones, karafuu na viungo vingine, magogo na mazao yanayotokana na hayo, vitu vya kupendezesha ngozi ya mwili (tanning/ dyeing extract). Takwimu zinazoonesha biashara kati ya India na Tanzania zimetolewa kwenye jedwali lifuatalo hapo chini.

### Jedwali 3.2: Biashara ya India na Tanzania (2008-2010[50])

| Mwaka | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|
| Uuzaji wa bidhaa kwenda India katika dola za kimarekani ( milioni) | 859.73 | 772.87 | 895.01 |
| Uagizaji wa bidhaa kutoka India katika dola za kimarekani ( milioni) | 171.82 | 187.58 | 226.19 |
| Jumla | 1031.55 | 960.45 | 1121.2 |

Chanzo: Wizara ya Mambo ya Nje, Serikali ya India (2011)

Takwimu imeonesha kwamba, kati ya mwaka 2004 na 2008, uuzaji wa bidhaa za Tanzania kwenda Urusi uliongezeka kutoka Tshs bilioni 1.41 hadi Tshs 5.985 wakati huo huo, uuzaji wa bidhaa toka Urusi kuja Tanzania ulishuhudia ongezeko kutoka Tshs bilioni 2.3 hadi Tshs bilioni 87.82. Kwa maoni ya aliyekuwa waziri wa viwanda na biashara, Dr. Mary Nagu, hali hii inaashiria kwamba kuna fursa kubwa ya kukua kwa biashara kati ya nchi hizi mbili hadi kufikia kiwango kikubwa zaidi.

49 Kaijage F (2013) Ripoti ya Siri ya Ujangili inayotuhumu China. Imepatikana tarehe 18.05 katika tovuti ya http://www.ippmedia.com/frontend/21=54837

50 www.mea.gov.in/meaxpsite/mahusiano ya nje/tanzania.pdf. Imepatikana 12/12/2011

Hata hivyo, Tanzania pia inapaswa kurekebisha ufa wa uwiano wa kibiashara uliokuwa umefikia Tshs milioni 866 mwaka 2004 hadi Tshs bilioni 81.8 mwaka 2008 na kuipa Urusi fursa ya kuinuka[51]. Kutokana na takwimu zilizooneshwa katika jedwali namba -1, huo ufa wa uwiano wa kibiashara hauonekani kupungua hata baada ya mwaka 2008.

Kwa upande wa Afrika Kusini, yenyewe ndiyo inashika nafasi ya tatu katika kuuza bidhaa zake Tanzania ikiwa inatawala soko kwa asilimia 9.63%. hata hivyo, wakati ambapo uuzaji wa bidhaa za Afrika Kusini kuja Tanzania umepungua kiasi fulani kutoka dola za Marekani milioni 500 mwaka 2009, ununuzi wa bidhaa kutoka Tanzania umeongezeka kwa karibu asilimia 100%,kutoka dola za Marekani milioni 22 mwaka 2009 hadi dola za Marekani milioni 44 mwaka 2010. Kwa sasa, bidhaa kuu ambazo Afrika Kusini inaiuzia Tanzania ni: bidhaa za viwandani kama vile mitambo (mashine), vifaa vya magari, karatasi, mazao yatokanayo na mpira, magari, chuma, chuma cha pua, huduma na teknolojia. Bidhaa inazoziagiza kutoka Tanzania zaidi ni dhahabu, kahawa, korosho na pamba[52].

Biashara kati ya Brazil na Afrika imeongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 2 mwaka 2000 hadi dola za Marekani bilioni 12 mwaka 2010. Bado kuna shida ya usafiri (wa majini na wa anga), teknolojia ya habari na mawasiliano (teknohama) na kasi ya taarifa ni miongoni mwa mambo mengine yanayochangia kudidimiza kasi ya ukuaji wa kiwango cha biashara. Hata hivyo, kuna matarajio kwamba hali hii itabadilika katika kipindi kifupi na cha kati kwa kuwa uchumi wa Afrika unazidi kukua na kadiri uchumi wa Brazil unavyozidi kupanuka sambamba na shauku yake kwa ajili ya rasilimali za Afrika. Makampuni ya Brazil yamekuwepo katika Afrika tangu miaka ya 1980 hususan katika nchi zinazozungumza kireno. Hivi sasa yapo katika nchi zinazozungumza kiingereza na kifaransa, zikiwekeza katika miundombinu, madini, mafuta na nishati[53].

Katika hatua nyingine, mahojiano kati ya balozi wa Brazil nchini Tanzania na gazeti la the citizen[54], yamedhihirisha kwamba, biashara kati ya nchi hizi mbili zimekiuka utaratibu ili kuipa upendeleo Brazil. Mwaka 2011, ilifikia dola za

51 http://www.tanzaniainvest.com/industry-trade/news/347-improved-tanzania-trade-relations-with-russia-sought [ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

52 Tarakimu ya Uuzaji bidhaa nje kwa mwaka 2010 haikutolewa na chanzo husika. http://www.southafrica.info/news/international/tanzania-200711.htm#.UQo6Lr-TxPI#ixzz2JXwHvV6U[ ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

53 Benki ya Dunia na Taasisi ya Utafiti wa kiuchumi cha Brazil (2010) kuziba pengo la Atlantic: Brazil na Nchi zilizo kusini wa Jangwa la Sahara na umoja wa ushirikiano Nchi zilizo kusini mwa Afrika wakishirikiana kwa ukuzaji uchumi Benki ya Dunia: Washington.

54 Chanzo hakikutajwa (2012) jinsi ambavyo Tanzania inaweza kuupunguza umaskini. Gazeti la the Citizen la tarehe 01 Julai Inapatikana katika: http://www.thecitizen.co.tz/sunday-citizen/41-sunday-citizen-business/23649-how-tz-can-reduce-poverty.html [ ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

Marekani milioni 76. Wakati wa mahojiano hayo yaliyofanyika tarehe (01/07/2012), Tanzania ilikuwa imeshauza bidhaa hasa tumbaku yenye thamani ndogo sana, kiasi cha dola za Marekani 7,000 (karibu shilingi milioni 11.2). kwa upande mwingine, ununuzi wa bidhaa kutoka Brazil ikiwemo sukari , spea za magari na kuku vilikuwa na thamani ya dola za Marekani miloni 20 (Tshs bilioni 32). Brazil pia inaagiza bidhaa za kawaida kutoka nchi nyingine, bidhaa kama vile karafuu, katani na mafuta ya nazi ambayo pia yanapatikana Tanzania.

Uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na BRICS umekuwa na matokeo ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja kwa uchumi wa Tanzania. Matokeo ya moja kwa moja yanajumuisha kuongezeka kwa mauzo ya nje na kuongezeka kwa bei za mali ghafi zinazouzwa nje hadi bidhaa zinazouzwa nje kufikia idadi kubwa ya wahitaji na kuboresha maisha yao. Hata hivyo jinsi dhana hii itakavyopunguza umasikini inabakia kuwa tata. Hata hivyo, kuongeza kwa ukuaji wa bidhaa nje kuna mabadiliko chanya katika kuondoa umasikini kama utazingatia kukuza uwekezaji, kukuza ongezeko la matumizi, kuongeza ajira na kupanua wigo wa uzalishaji. Hili litaongeza kipato cha mtu. Mdahalo juu ya kuingiza bidhaa za BRICS Tanzania umegawanyika. Kwa upande mmoja, mchanganuzi mmoja alidokeza kwamba watazamaji wanaweka hali ya kutokuwa na imani na kanuni ya soko huria kama mtu akija akakuonesha kitu anachotaka kukuuzia, unaweza kuamua kama utakinunua au la, hii ni sawa[55].” Huko ni kubadilishana kwa haki. Katika upande mmoja bidhaa hizi zinazoingizwa, zinaleta changamoto kwa uchumi wa Tanzania.

Mwandishi wa UK Sunday Times Bwana Swains, Mwaka 2008 aliripoti kuwa uuzaji wa bidhaa za malapa (sandals) kwendanje unakufa. Miaka michache iliyopita, uuzaji wa malapa kwenda nje uliajiri watu 3,000 na uliuza bidhaa hii sehemu mbalimbali za bara. Sasa inaajiri watu 1,000. Meneja wake wa kilebanoni alilalamika kwamba hawezi kushindana na bidhaa rahisi za kichina zinazouzwa chini ya gharama za uzalishaji. Mwandishi huyo huyo alilalamika kwamba wachina wamekuwa wakisafirisha bidhaa katika makontena ya kidiplomasia katika ubalozi wake wa Dar es Salaam, wakikwepa ushuru wa forodha na kodi ya bidhaa zinazoingia ndani , jambo ambalo linaweza kuwa hadithi ya kubuni tu. (Swain, 2008[56])

Katika taarifa nyingine inayohusiana na hiyo, utafiti uliofanywa na Mashindano na wengine mwaka 2007 unaonesha kuwa China inaongoza kwa kuingiza bidhaa bandia nchini Tanzania. Inafuatiwa na India, Umoja wa Falme za Kiarabu U.A.E (Dubai) na Kenya. Bidhaa bandia zinaathiri uchumi kwa njia tofauti. Njia hizi ni

55 Schroder R ( 2008) marejeo ya kisosiolojia ya Afrika 12, 1, 2008,ukurasa wa.20-34
56 Swain, J (2008) Afrika, kimbilio mpya la China, Gazeti la The Sunday Times, Februari 10, 2008, inapatikana katika:http://www.timesonline.co.uk/tol/news/world/africa/article3319909.ece, [ ilitembelewa tarehe 25/05/2008

pamoja na, kupoteza mapato ya serikali, kupoteza fursa za ajira, madhara ya kiafya (magonjwa na vifo), kuongezeka kwa umasikini, uwiano usio sawa wa kibiashara unaodhoofisha uzalishaji wa ndani, (Moshi na Mtui, 2008). Kwa kawaida suala la bidhaa bandia kutoka China zinazoingizwa Tanzania limekanushwa na mamlaka za China. Machi 2012, Balozi wa China akiwa Dar es Salaam alikanusha habari hizo na kuahidi kwamba Serikali yake itashugulikia suala hilo kwa juhudi zote. (Masare, 2012)

Serikali ya Tanzania na wadau mbalimbali wamechukua hatua mbalimbali kutatua suala la bidhaa zinazoingizwa ndani. Hizi zinajumuisha lakini siyo hizi tu zifuatazo: mamlaka za udhibiti, kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamalaka ya Mapato (TRA) na Shirika la Viwango (TBS) na shirika la wenye viwanda nchini (CTI) wameweka juhudi za

Uraghabishi za kuendesha kampeni dhidi ya bidhaa zisizokidhi viwango katika soko la ndani. Juhudi hizi zinaambatana na mikakati ya kupitia upya sheria na taratibu zitakazozipa nguvu mamlaka za udhidhibiti kutatua kwa ufanisi tatizo hilo kuliko lilivyo hivi sasa (Moshi na Mtui, 2008)

## 4.0 UWEKEZAJI

Moja ya wadau muhimu katika uwekezaji toka nje katika Afrika ni China. China ni moja kati ya nchi kuu tano katika uwekezaji hapa Tanzania (Tazama jedwali 4.1), lakini inafanya uwekezaji hasa katika viwanda, uchimbaji madini, ujenzi, utengenezaji wa nguo, na kilimo. Kwa mfano kama ilivyoripotiwa na ubalozi wa China (2008), kufikia mwsho wa mwaka 2008, kulikuwa na miradi ya uwekezaji 224 ya Kichina hapa Tanzania katika sekta zifuatazo: Viwanda (163), Ujenzi(21), Utalii(11), Usafirishaji(7), Huduma(7), Kilimo(6), maliasili(6), na Teknohama (3)[57]

Mfano mwingine muhimu ni wa kiwanda cha kusindika asali (Honey King Limited) ambacho kilizinduliwa mwaka 2012 na Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Pinda, ambacho kina uwezo wa kusindika tani za metriki 10,000 za asali kwa mwaka. Kinatoa utaalamu kwa wafugaji wa nyuki ili waweze kuzalisha asali ya asili kwa masoko ya Marekani, Ulaya na Mashariki ya Kati (Majaliwa, 2012[58]). Hili si jambo la kustajabisha kwa kuwa China ni moja ya wazalishaji wakuu wa asali duniani[59].

---

57 http://www.tanzaniaembassy.org.cn:8081/index.php?option=com_k2&view=item&id=51:growing-and-thriving-together-china-and-tanzania&tmpl=component&print=1&lang=en

58 Majaliwa M (2012) kiwanda cha china kimefunguliwa: Gazeti la Daily News online. http://dailynews.co.tz/index.php/local-news/6063-chinese-honey-factory-opened [ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

59 http://www.vsjf.org/assets/files/Agriculture/Strat_Plan/3.3_Honey%20Production_11.11.pdf [ilitembelewa tarehe 01/02/2013]

Li na wenzake (2010)[60], walifanya utafiti juu ya sababu zinazochangia kukua kwa kasi kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wa China (Chinese FDI) katika viwanda vya maliasili hapa Tanzania. Kutokana na mahaojiano na makampuni ya ujasiriamali ya kimataifa ya China (Chinese multinational enterprises (MNEs), utafiti ulidhihirisha matokeo mawili makubwa yafuatayo:

Matokeo ya kwanza yanahusiana na serikali ya nyumbani, kwa maana ya serikali ya China imekuwa chachu katika kuwezesha uwekezaji nje ya nchi kwa makampuni ya kichina katika namna mbili muhimu.

Kwanza, Serikali ya China inaingia katika makubaliano ya kiuchumi na nchi husika (kwa mfano, kupitia majukwaa ya kiuchumi, na mikopo inayodhaminiwa na mali kwamba Nchi za Afrika zinaweza kutumia maliasili kama dhamana kwa mikopo kwa jili ya miradi ya ujenzi kwa nchi zenye miundombinu hafifu) na katika kujadiliana na serikali ya nchi husika juu ya uwekezaji katika viwanda vya maliasili. La pili:

Serikali ya China hutoa moja kwa moja, msaada wa thamani kwa makampuni ya nyumbani katika viwanda vya maliasili ambayo inajumuisha sio tu taarifa muhimu za uwekezaji,bali pia msaada wa fedha na sera kwa makampuni yake yanayowekeza Afrika. Mikakati hii inasaidia makampuni (ambayo yanakosa fursa za ushindani wa teknolojia na jina la biashara) kushindana na makampuni mengine duniani. Utafiti unadhihirisha kwamba Makampuni ya Kichina yanapaswa kujua kwamba baada ya kupata misaada ya kifedha na taarifa za uwekezaji kutoka serikali ya China, lazima walipe fadhila kwa serikali kwa kukubali kuingiliwa na Serikali katika maamuzi[61]. Hata hivyo mkakati huu ukitumika kwa muda mrefu, utaongeza utegemezi wa kulindwa na Serikali na kudhoofisha ubunifu katika uzalishaji wa ushindani na fursa za ushindani katika biashara ya kimataifa.

Matokeo ya pili katika utafiti unahusiana na makampuni ya kichina yanayoongoza katika viwanda vya maliasili ambavyo vinaonesha miradi yenye manufaa zaidi ya moja katika miundombinu, viwanda, viwanda vyenye mwelekeo wa kilimo, afya, na elimu kulingana na mahitaji yaliyobainishwa na watanzania. Viwanda vya maliasili havina uwezo wa kutoa huduma peke yake katika sekta zote, kwa hiyo vinaungana na makampuni mengine na kuunda ubia. Kwa mwongozo na msaada wa Serikali ya China, makampuni ya kichina yameungana ili kutoa bidhaa na huduma zinazokidhi mahitaji mengi ya watanzania.

[60] Li A, Newenham-Kahindi A na Shapiro D. M ( 2010) uwekezaji wa moja kwa moja kutka nje katika viwanda vya maliasili katika Afrika.:Wachina dhidi ya wafanya biashara wa ulaya magharibi makala ya uchambuzi katika kituo cha Jack Austin, uchambuzi wa masuala ya biashara kwa Asia na Pacific, Chuo Kikuu cha Simon Fraser. Inapatikana: http://business.sfu.ca/jack-austin-centre/wp-content/uploads/2011/09/Working-paper-China_investment_in_Africa.pdf [ ilitembelewa tarehe 17/05/2012]

[61] Baada ya kupokea misaada na rasilimali kutoka kwa serikali, makampuni yanatakiwa kuruhusu serikali kupata taarifa za makampuni kama njia mojawapo ya kurudisha shukrani

Kuhusu India, kutokana na takwimu zilizopatikana kutoka kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC- jedwali 4.1 ) kutoka 1990-2011, India inaongoza miongoni mwa kundi la BRICS.

**Jedwali 4.1: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC): Usajili wa miradi kwa nchi kumi zinazoongoza mwaka 1990-2011**

| Nafasi | Nchi | Miradi | Kazi | Thamani ( kwa Dola Milioni za Marekani ) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uingereza | 925 | 254131 | 2039.87 |
| 2 | Uholanzi | 159 | 14174 | 1895.78 |
| 3 | India | 305 | 42905 | 1546.56 |
| 4 | Kenya | 428 | 48942 | 1425.56 |
| 5 | China | 373 | 60329 | 1027.84 |
| 6 | Marekani | 194 | 40360 | 858.10 |
| 7 | Afrika Kusini | 191 | 17228 | 647.09 |
| 8 | Canada | 177 | 24045 | 481.85 |
| 9 | Ujerumani | 140 | 14114 | 284.99 |
| 10 | Oman | 34 | 1565.05 | 217.76 |
| 65 | Urusi | 24 | 979 | 25.69 |

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (2012)

## N.B Makampuni ya Brazil hayajasajili uwekezaji wake na TIC.

Kuvutia kwa Tanzania kwa wawekezaji wa ndani na wa nje kunaathiriwa na hali ya kibiashara isiyo rafiki. Mwaka 2011, Tanzania ilishuka na kurudi nyuma nafasi mbili (kutoka nafasi ya 125 mwaka uliopita hadi 127) katika orodha ya ufanyaji biashara duniani. Tathmini zaidi zilionesha kuwa uendeshaji wa biashara Tanzania hauendani na mabadiliko yanayoedelea sasa. Licha ya hivyo, Tanzania inaonekana kuwa chini ikilinganishwa na nchi nyingine katika ukanda huu kama Rwanda, Kenya na Uganda (World Bank and International Monetary Fund, 2012[62]) na hivyo kukatisha tamaa wawekezaji wanaotarajia kuwekeza. Sababu za kuwekwa chini katika orodha ni urasimu katika uanzishaji wa biashara, kushugulikia leseni, mazingira ya ushindani huru, kuajiri wafanyakazi, kuandikisha mali, kupata mikopo, kulinda wawekezaji, kulipa kodi, biashara nje ya mipaka, utekelezaji wa mikataba, wanawake katika jamii, kuendana na hali ya hifadhi ya chakula na

[62] Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani ( 2012) Kufanya Biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (2012), Washington

jinsi ya kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa. Zaidi ya hapo, kutokuwa na umeme wa uhakika kumeshutumiwa na waendeshaji wengi wa viwanda, suala ambalo limezingatiwa katika kutathmini uwezo wa kiushindani wa nchi kuvutia wawekezaji.

Pamoja na changamoto hizo, India bado ni mbia muhimu kwa Tanzania kwenye sekta ya kilimo kwa sababu zifuatazo;

Kwanza, Tanzania inahitaji Mapinduzi ya Kijani ambayo yamekuwa ndiyo msingi mkuu wa mafanikio ya kilimo India, kuibadilisha nchi kutoka moja ya nchi zenye uhaba mkubwa wa chakula hadi kujitosheleza yenyewe kwa chakula.

Pili, uwekezaji katika sekta binafsi India umejikita katika nchi ambazo kuna raia wake wengi[63]. Hata hivyo, mkakati huu unabadilika kwa kasi kwani kwa sasa wanatafuta sehemu za tofauti za kuwekeza. Mfano ni Export Trading Group ambao makao yake makuu yapo Dar es Salaam, Tanzania[64]. Shughuli kubwa za kikundi hiki ni kwenye kilimo ingawa uwekezaji wa pamoja[65] pia wapo kwenye teknolojia ya mawasiliano, uchimbaji madini, utalii, misitu, usafirishaji, na bandari.

Tatu na ambayo inaendana na hiyo hapo juu, utafiti wa biashara Africa umeonesha kwamba mitandao ya kibiashara India imeungana pamoja kwa kupeana taarifa, kushirikisha mawasiliano, mara nyingine kupeana mikopo, na kuaminiana (ambako kunasaidiwa na makubaliano waliyojiwekea). Kwa maneno mengine, wamebeba jukumu muhimu la kukuza sekta binafsi katika bara la Afrika kwa kuleta ubunifu na mbinu nzui zaidi, rasilimali fedha na fursa za mitandao (Brautigham, 2003[66])

Kadhalika, jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya miradi ya kilimo kuanzia mwaka 1990-2007[67]. ambayo "India ina maslahi nayo." Vile vile inaonesha kwamba kuna makampuni ya India, ambayo yamewekeza sekta ya kilimo ambayo mara nyingi huwa hawapewi wageni nao wanatumia kiasi kikubwa cha malighafi moja kwa moja kutoka mazao ya kilimo.

63 Uwekezaji kutoka India ama uwekezaji wenye manufaa kwa India unarejewa kwa uhuru hapa na penginepo kama uwekezaji kutoka (i) raia wa India wenye viza za India ambao hawaishi Tanzania. (ii) watanzania wenye asili ya India ambao kabda walikuwa raia wa India au ambao wenza wao, wazazi, mababu, baba wa babu waliwahi kuwa raia wa India

64 Mahojiano yaliyofanyika na maafisa wa ETG, Desemba 2010.

65 Nchi nane za Afrika Magharibi, Mashariki, Kusini, Pembe ya Afrika, India na Umoja wa Falme za Kiarabu

66 Brautigham D (2003) Ujasiriamali wa ndani Kusini Mashariki mwa Asia na Kusini mwa Jangwa la Sahara: Mitandao na Mwingiliano na Uchumi wa Dunia Asia na Afrika (Eds, Aryeetey E, E court, J. Nissanke, M na Weder, B) United Nations University Press, New York, PP 106-127: Ramachandran V na Shah M.K (1998) Wajasiriamali wachache na utendaji wa kampuni kusini mwa Jangwa la Sahara, Benki ya Dunia, RPED chapisho la sita 86

## Jedwali 4.2: miradi iliyochaguliwa ya kilimo iliyosajiliwa na kituo cha uwekezaji Tanzania ambayo "India ina maslahi nayo"zikiwemo shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo kuanzia mwaka 1990-2007[68]

| Jina la Mradi | Shughuli za Kilimo | Idadi ya Waajiriwa | Uwekezaji wenye thamani ya ( dola za Marekani milioni) |
|---|---|---|---|
| Arusha Farms Ltd. | Shamba la katani | 407 | 0.54 |
| Tan Farms Ltd. | Shamba la katani | 385 | 0.37 |
| Tanagri Ltd. | Kilimo cha papai | 15 | 0.74 |
| The Bombay Burmah Trad. Corp. | Kilimo cha chai | 147 | 0.39 |
| Mayambe and Digoma Farms Ltd. | Kilimo na ufugaji | 85 | 0.02 |
| Tanzania Plantations Ltd. | Mazao ya kilimo & mifugo | 197 | 0.38 |
| Euro Vistaa (T) Ltd | Ukulima wa mashamba ya biashara | 450 | 27.77 |
| Mega Cashewnuts & Allied Plant. | Mashamba ya korosho | 205 | 1.80 |
| Shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo | | | |
| Coastal Millers Ltd | Wasaga unga wa nafaka | 30 | 2.57 |
| Sun Cape | Mafuta ya kula | 70 | 2.44 |
| NSK (T) Ltd. | Mafuta ya kula | 73 | 1.51 |
| Nipha Pamba Engineering Co. Ltd. | kinu | 86 | 5.07 |
| Nipha Pamba Ltd. | kinu | 59 | 2.13 |
| M. A. Kharafi (T) Ltd. | ubanjuaji wa korosho | 100 | 1.75 |
| Mega Cashewnuts & Allied Plant. | Ubanjuaji wa korosho | 223 | 8.47 |
| Bidco Tanzania Ltd | Kiwanda cha kusafisha mafuta | 500 | 3.33 |
| Olam Tanzania Ltd | Usindikaji wa korosho | 3730 | 10.15 |
| Bake Food International Ltd | kiwanda ya uokaji | 200 | 1.16 |
| Indo-African Essential Oils | Uchimbaji wa mafuta muhimu | 120 | 2.59 |
| Mount Meru Seeds Ltd | Kiwanda cha kusindika mbegu | 52 | 1.41 |

Source: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (2010)

67 Zile tu zilizotengenezwa kupitia kituo cha uwekezaji ndizo zinazofaidika na motisha maalum ya uwekezaji

Kupitia kauli ya KILIMO KWANZA ya Tanzania, mwito mpya wa juhudii za kufufua kilimo, kuna idadi ya maeneo mapya ya uwekezaji kwa India au kwa kushirikiana yanapangwa, Eneo moja ni la ubanguzi wa korosho Tanzania, ambalo lilikuwa limehamasika kwenye miaka ya 1970 ambapo zaidi ya viwanda 25 vilikuwa vimeanzishwa kama mali ya umma, huku baadhi ya mitambo ikiwa imetolewa India. Kuanguka kwa mfumo wa viwanda Tanzania katikati ya miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990 kuliacha idadi kubwa ya viwanda hivi kwenye hali mbaya na vingine vikiwa havifanyi kazi kabisa. Tokea ubinafsishaji ulipoanza kwenye muongo wa mwisho, dhamira imekuwa kuanza au hata kukarabati viwanda vya utengenezaji, ambako matumizi ya teknolojia ya India imekuwa ikitafutwa. Kwa sasa, zaidi ya asilimia 40 ya korosho inayozalishwa Tanzania inasafirishwa kabla ya kubanguliwa kupelekwa kwenye soko la India, na kiasi kidogo kikipelekwa Kenya na Pakistan (UNIDO, 2011, UNCTAD/WTO 2002[69]). Inapofika huko, inasindikwa kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu na kusafirishwa tena kwa wasindikaji wakubwa na wasambazaji kwenye nchi zenye viwanda vingi[70], na hivyo kuongeza thamani na ajira nje ya Tanzania.

Pamoja na hayo, mvuvumko na uthabiti wa nguvu ya India kiuchumi unaonekana sasa hivi Tanzania kwa kupitia uwekezaji mkubwa, unaofanywa na Kamal Group ya India, ikiwa na mpango wa kutumia shilingi bilioni 327 (dola milioni 213) kuanzisha kiwanda cha chuma Tanzania[71]. Kiwanda hiki, ambacho kitakuwa kikubwa kuliko vyote Afrika ya Mashariki, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha kiasi cha tani mita 700,000 za chuma kwa mwaka.

Kwa nchi nyingine za BUICAK, kutokana na mwenyekiti wa Chinese Business Chamber, Tanzania itavutia uwekezaji zaidi kutoka China kama itashughulikia masuala ya usalama na kuboresha miundombinu (Masare, 2012[72])

Kwa upande wa uwekezaji wa Afrika ya Kusini, umekuwa ukikua polepole tokea kumalizika kwa siasa ya ubaguzi wa rangi mwaka 1994. Kutokana na jedwali

68 Mutalemwa, D K. na Mutalemwa, D P. (2011) Engaging Tanzania Africa Quarterly,.Toleo la 51 namba 3-4. Ukurasa wa 94-101.

69 UNIDO (2011). Tanzania's Cash Value Chain: A diagnostic. Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia maendeleo ya viwanda. Vienna, Austria; UNCTAD/WTO (2002). Tathmini ya hali halisi na matarajio ya maendeleo kwa ajili ya sekta ya korosho www.unctad.info/upload/information/Docs/cashew/tanzania.pdf, Accessed 03/04/2013

70 Mkakati wa Afrika kwa ajili ya maendeleo ya Biashara na Kilimo na Bisahra na Viwanda

71 Vyanzo: Ubalozi wa India

72 Mwenyekiti alisema "katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kumekuwa na mfululizo wa matukio ya wizi wa kutumia silaha ukiwalenga wawekezaji wa kichina, akiwemo mwanamke aliyeuawa mwezi Octoba mwaka jana. Tunafikiri serikali inapaswa kulipa suala hili uzito unaostahili ili kuboresha mazingira ya biashara kwa wawekezaji wa kichina na wengine hapa nchini''. Aliongeza kuwa barabara nyembamba ambazo mar azote husababisha foleni kubwa ya magari yamekuwa changamoto kwa wawekezaji wa kichina kwa kuwa yanachelewesha shughuli za biashara.

4.1, Afrika ya Kusini ilishika nafasi ya 7 kwa kiasi cha uwekezaji kilichosajiliwa na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji mwaka 2012, ukiwa na thamani ya dola za Marekani 858.10. Kwa jumla, uwekezaji wa Afrika ya Kusini nchini Tanzania ni pamoja na huduma za usafiri wa anga (kwa mfano South African Airways), uzalishaji katika viwanda (kwa mfano. SAB Miller Tanzania Breweries), huduma za kibenki na fedha (mfano. Stanbic Bank; rejareja (mfano. Shoprite, the Game, Steers); mawasiliano (mfano. Vodacom), habari na utangazaji (mfano. Multichoice); utalii na starehe (mfano. Protea, Southern Sun) kwa kutaja tu machache.

Pamoja na kumbukumbu hii, afisa wa juu kutoka Kituo cha Taifa cha Uwekezaji, ambacho kazi yake kubwa ni kukuza uwekezaji kutoka nje, hakuficha hisia zake alipokaririwa akisema;

"Wawekezaji wote wa Tanzania na Afrika ya Kusini wanatakiwa kuwa makini kwa sababu tuko kwenye hali ambayo mtindo wa kufanya kazi Afrika Kusini unaweza ukatafsiriwa kama udhalilishaji Tanzania…..Wawekezaji wengi kutoka Afrika Kusini ni weupe. Ikitokea kitu chochote kikatokea kwenye eneo la kazi, wafanyakazi wa kitanzania wanakumbuka siasa za ubaguzi wa rangi Afrika Kusini. Ninadhani tunatakiwa kuwaelimisha watu wetu na wawekezaji pia wanatakiwa kutumia muda wao kusoma utamaduni wa watanzania". (Rwambal na wenzake, kutoka Schroder, 2008).

Baadhi ya uwekezaji wa Afrika Kusini uliojipambanua zaidi Tanzania ni pamoja na maduka ya jumla, Shoprite ambao waliingia mwaka 2000 wanahitaji kutajwa. Wamelaumiwa sana kwa kuleta nchini bidhaa ambazo zinapatikana hapa hapa.

''Uwekezaji (wa Afrika Kusini)… haunufaishi watanzania; kwamba kila kitu kinatakiwa kutoka Afrika Kusini – huo sio uwekezaji hata kidogo. Kwa kiasi kikubwa wamekuja kuua biashara yetu. Hata pale mfanyabiashara wa kike anapotaka kuuza nyanya, hawezi kwa sababu tayari kuna nyanya zimeletwa kutoka Afrika Kusini. Kwa uwekezaji huo, wanataka kutudanganya. Mwanzoni tulidhani wamekuja Tanzania kushirikiana nasi kuuza bidhaa zetu ili tupate faida. Ndipo tumekuja kugundua kwamba wamekuja kufungua maduka na kuuza bidhaa kutoka nchini kwao, bila hata kutaka kuangalia kinachozalishwa hapa ndani. Huo sio urafiki hata kidogo. Ni sawa na mtu kuja kufanya ubaguzi kwenye nchi yako. Wakati anapokuja mtu kwenye nchi yako na hataki hata kuangalia bidhaa zako, ni kama anakutukana. Ni udhalilishaji''. (Mfanyakazi wa maendeleo 1, imetolewa kwenye Schroder, 2008[73])

[73] Schroder R (2008) Marejeo ya Kisosiolojia 12, 1, 2008, pp.20-24

Serikali ya Tanzania kwa muda mrefu sasa imetoa wigo mpana wa motisha wa kodi ukiwa na lengo la kuvutia na kubakisha kiasi kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kuja Tanzania. Hata hivyo, kumekuwa na hoja zinazoongezeka kila mara kuwa chanzo kikubwa cha uwekezaji wa nje kwa BUICAK ni mapumziko ya kodi[74], ambayo mara nyingi yanajulikana kama vituo vya fedha vya nje. Matumizi ya mapumziko ya kodi sio haramu, ila usiri uliopo kwenye biashara kwenye hizi mamlaka zenye kodi za chini na vyombo vinavyo anzishwa, inaruhusu kiasi kikubwa cha fedha kufichwa kwa umma, na inawezesha makampuni na watu matajiri kukwepa kulipa kodi na kuzileta fedha hizi nchini kama uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Utafiti uliosimamiwa na Interfaith Standing Committee on Economic Justice and the Integrity of Creation in Tanzania, ulionesha kuwa mengi ya makampuni makubwa yanayondesha shughuli zake Tanzania yanatumia mapumziko ya kodi kwenye muundo wao wa kiutendaji mfano. Vodacom na SAB Miller Tanzania Breweries[75] ikimaanisha upotevu wa mapato ya kodi.

Pamoja na changamoto hizi, BUICAK ni chanzo muhimu za uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ambao unahusishwa na athari nyingi chanya kwenye uchumi. Hii inajumuisha pamoja na mambo mengine yafuatayo (Moshi na Mtui, 2008:18): (i) utengenezaji wa mtaji kwa kupitia upatikanaji wa rasilimali fedha; (ii) Uhamishaji wa teknolojia, kwa njia ya bidhaa zinazotengenezwa kama mitambo, vifaa na vitendea kazi, na ujuzi kama utawala na usimamizi wa shirika, masoko, nk; (iii) Upatikanaji wa masoko ya nje mfano. Kiwanda cha URAFIKI ambacho kinamilikiwa kwa pamoja kati ya China na Tanzania, kikiuza nje kiasi kikubwa cha bidhaa zake; ukuzaji wa ushindani wa ndani ambao unaongeza ustawi wa jamii kwa kupitia upatikanaji wa bidhaa, uboreshaji wa ubora, na punguzo la bei; (iv) Upatikanaji wa ajira na mapato, na hivyo kuchangia kupunguza umaskini wa kipato na kusaidia bajeti ya Serikali.

## 5.0 UHAMIAJI

Katika karne ya 19, wahamiaji wengi waliohamia Afrika Mashariki wa aina ya wafanyabiashara, wavumbuzi, wamisionari, na askari, walitokea Ulaya Magharibi. Mbali ya makundi haya, katika Afrika Mashariki na hususan Tanzania, wahamiaji wa Kihindi wanaweza kuwa kundi kubwa kuliko yote. Lakini walikuwa ni wafanyakazi wa mikataba wa mamlaka ya reli ya Kenya, na wafanyakazi wa kati na chini katika utawala wa kikoloni.

[74] Hakuna tafsiri sahihi ya mapumziko ya kodi. OECD mwanzoni walitafsiri sifa zifuatazo za mapumziko ya kodi: kodi kidogo au hakuna kabisa, hakuna ubadilishanaji wa taarifa, hakuna wazi na uwajibikaji.

[75] Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Umoja wa Makanisa ya Kikristo Tanzania (CCT) Hilo swali la Dola Bilioni Moja: Je, Tanzania inawezaje Kuacha Kupoteza Kiasi kikubwa Namna Hiyo ya Mapato Yatokanayo na Kodi?.

Sababu kadhaa zinaelezea madhumuni ya Wachina kuhamia Tanzania na nchi nyingine za Afrika kuanzisha biashara (Rodrick, 2007[76]). Kwanza, utamaduni: wachina kwa asili ni wajasiriamali na hivyo wanaweza kuona fursa na kujinufaisha hata kwa fursa za wafanyabiashara wadogo kabisa ambazo wazawa wanazichangamkia. Pili, Mtandao:  kumekuwa na ongezeko kubwa la uwekezaji wa Kichina katika madini ya Afrika na rasilimali nyingine za asili. Hii inavutia aina nyingine za shughuli za kiuchumi katika bara (spill-over and coattail riding investments). Tatu, kuchagua: wale watu wanaoamua kutoka China kutafuta fursa za kiuchumi Afrika wanaonekana kuwa wajasiriamali zaidi na wenye kujitoa muhanga kuliko wachina wa kawaida. (na hata waafrika wa kawaida). Mwisho, ufahamu: Wajasiriamali wa kichina wanao uzoefu wa kufanya biashara katika njia za kificho au rushwa/ mazingira yasiyotilia mkazo kisheria. Wanao uwezo wa kuutumia uzoefu huu katika muktadha wa kiafrika, ambao una sifa nyingi zinazofanana. Dhana ya 'spill over' ina sifa ya kipekee kwa Wafanyakazi wenye taaluma wa kichina kwa kazi za miundombinu na ujenzi: idadi kubwa hawarudi nyumbani baada ya kumaliza mikataba yao ya awali kwani hupata mikataba mingine ndani  ya nchi kwa kushinda tenda kwa njia ya ushindani wa wazi kwa sababu ya unafuu wa gharama na uaminifu katika kazi. (Centre for Chinese studies, 2007[77]). Au wanatumia uzoefu wao wa hali ya biashara ya ndani kuingia katika biashara zingine ambazo sio lazima ziwe za ujenzi.

Mung(2008) alivyonukuliwa katika Arsene (2010[78]) aligundua aina tatu za wahamiaji wa kichina wanaokuja Afrika;Wahamiaji wa muda wanaofanya kazi katika miradi inayofadhiliwa na Serikali au miradi iliyotolewa kwa makampuni makubwa ya Kichina(ujenzi wa miundombinu, majengo ya umma, viwanja vya michezo vyaTaifa, viwanja vya ndege, n.k); Wahamiaji wapitaji wanaofanya kazi Afrika kwa muda ambao wana matarajio ya kukaa Ulaya au Amerika ya Kusini; na wajasiriamali wadogo wanaokuja Afrika mara nyingi kibinafsi bila kutegemea serikali ya China.

Kuhusiana na aina hii ya mwisho ya wahamiaji, mmoja wa wahamiaji wa kichina ambaye familia yake ilihamia Tanzania mwaka 2008, alieleza kwamba yeye na familia yake waliamua kuanzisha gereji ya kutengeneza magari kwa kuwa walifahamu ya kuwa:

---

76 Rodrick, Dani (2007) Wafanyabiashara wa kichina Afrika, http://rodrick.typepad.com/dani rodriks weblog/2007/08/chinese-entrepr.html,( ilipatikana 12/12/2011)

77 Kituo cha Mafunzo ya Kichina (2006) Maslahi ya China na Kazi katika Sekta ya Ujenzi na Miundombinu Afrika. Chuo Kikuu cha Stellenbosch: Afrika Kusini

78 Arsene C (2010) Wachina Kuja Afrika: Ushindani, Ushirikiano, Muingiliano na Kutegemeana; Mafunzo kutoka Tanzania; BA Thesis (Hons) Chuo Kikuu cha Chicago: chicago

“Tanzania haina ukomo wa kuendesha magari baada ya kunywa, jambo ambalo linasababisha ajali nyingi; na ajali nyingi zinatuletea sisi biashara zaidi. Japokuwa sisi ni wageni hapa, gereji yetu inajaa magari kila siku; wakati mwingine hatupati nafasi hata ya kuegesha magari yetu wenyewe. Hali ya usalama barabarani Tanzania ni mbaya sana. Watanzania hawana ujuzi wala mbinu za kukarabati magari yao wenyewe. Ndio maana kuna gereji nyingi zinazoendeshwa na Wachina. karibu gereji zote zinafanya biashara vizuri. Kuna magari mengi mno ya kukarabati!. “(Krugia, 2011[79])

Wahamiaji wa Kichina wawe halali au haramu, wanafanya kazi ya kilimo, biashara na ujenzi na wanafanya kila kitu kuanzia miradi mikubwa ya miundombinu inayofadhiliwa na serikali, ujenzi wa barabara na reli, hadi miradi midogo ya ujasiriamali ya kuuza bidhaa, gereji za kukarabati magari, nk. na wanashindana na wajasiriamali wa kitanzania. Kimsingi, utafiti uliofanywa mwaka 2009 na mamlaka za mkoa wa Dar es Salaam uligundua kuwa wajasiriamali wengi wa kichina walijihusisha na biashara zingine tofauti na zile walizoandikisha kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Wengi wao wanapigana vikumbo na watu wa kawaida (Dar es Salaam kama kwenye masoko ya Kariakoo, Sinza na Manzese) wakiuza viatu, makobazi, nguo za bei rahisi. Lakini bidhaa nyingi kati ya hizi zinasemekana kutengenezwa ndani ya nchi (Kamndaya, 2010[80]).

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa Dar es Salaam na Arsene (2010[81]) juu ya mtazamo wa watanzania juu ya wahamiaji wa Kichina ulileta mambo ya kusisimua yafuatayo:

Wakazi wengi wa Dar es Salaam kwa ujumla waliwaona wahamiaji wa Kichina kama wachapa kazi, wenye malengo thabiti (majibu 411/500); ambao wanaishi katika mazingira kama yao (399/500); na wenye uelewa wa mifumo ya kibiashara na masoko ya Afrika (368/500). Wahojiwa wengine, walisisitiza kwamba wahamiaji wa kichina wanaishi maisha magumu na ya kawaida kama sisi (393/500) “Hawaishi maisha ya anasa kama wazungu (119/500) au Wafanyakazi wa kichina wana nidhamu ya kazi kuliko dada zetu na kaka zetu”(78/500). Idadi kubwa ya Wahojiwa (267/500) walisifia hali ya wachina kukaa pamoja na kusaidiana. Wahojiwa wengine walionesha kuvutiwa na hali ya wahamiaji wa kichina kuwa na “moyo wa umoja” (57/500), “upendo wao kwa Wachina wenzao”(61/500), au kuwepo kwa Wachina wanaokaa jijini kunasaidia wachina wageni wanaokuja kujifunza maneno machahe ya Kiswahili (112/500).

---

79 Krugia N J (2011) Kuwepo kwa wachina nchini Tanzania: Wahamiaji na wawekezaji, katika jarida la Nexus la Asia ya Mashariki, Chuo Kikuu cha Duke, Durham

80 Kamndaya S (2010), Mtaalamu: Njaa ya China kwa Rasilimali za Afrika, The Citizen, 30 Januari, limetolewa http://www.thecitizen.co.tz/newe.php?id=17113 (17/05/2012)

81 Arsene C (2010) Wachina Kuja Afrika: Ushindani, Ushirikiano, Muingiliano na Kutegemeana; Mafunzo kutoka Tanzania; BA Thesis (Hons) Chuo Kikuu cha Chicago: chicago

Sababu nyingine inayofanya wazawa kuwakubali wahamiaji ni moyo wa kujinyima (329/500);"wengine wanaweza kushinda na chupa ya maji tu bila kula ili kuokoa fedha", alisema mhojiwa mmoja. "Wengine wanaweza kuvaa jozi moja ya viatu hadi kitakapokwisha kabisa" aliongeza mwingine. Wanatumia fedha zao vizuri sio kama mume wangu anayepoteza nusu ya mshahara wake katika pombe siku anapopata mshahara. "(cha ajabu ni jinsi wahojiwa 101 walivyojadili kuwakubali wachina kwa uwezo wao wa kutunza fedha kwa kutokunywa pombe; asilimia 87 ya wahojiwa hawa ni wanawake).

Licha ya maoni chanya hapo juu kuhusu wafanyakazi wa kichina, kumekuwa na maoni hasi kuhusu wachina katika nchi kadhaa za Afrika ikiwemo Tanzania na haya yanaweza kuhusishwa na usemi wa kichina : "Mchina mmoja ni nyoka, wachina wengi ni wadudu" Idadi kubwa ya wachina katika ushindani na biashara za ndani na miongoni mwao wenyewe, inaendelea kuongeza kauli za upinzani dhidi ya wachina, inaongeza uhalifu mdogo na uhalifu zaidi dhidi ya wachina, na kuongezeka kwa rushwa na ufisadi, hasa kwa baadhi ya wachina wenye mafanikio kujionyesha kwa fedha zao, katika mazingira ambapo wengi wa wazawa wanabakia kukosa ajira . (Park, 2009)

Suala hilo hapo juu ni marudio ya kile kilichotokea kwa wahamiaji wa kihindi katika Afrika Mashariki, baada ya mradi wa ujenzi wa reli kupitia Kenya hadi Uganda mwishoni mwa karne ya 20.

## 6.0 Matokeo ya Utafiti na Maudhui yake

Ubia wa Tanzania na BRICS umejawa na mambo mazuri yanayoonekana na madhaifu kadhaa yaliyofichika, ambayo ni:

- Miongoni mwa nchi zinazounda BRICS, kila moja inashirikiana na Tanzania kwa namna tofauti kabisa kulingana na mtazamo wa kipekee, maslahi, vipaumbele na viunganishi vya kihistoria. Hali hii inaonesha kwamba itachukua muda kabla msingi unaowaunganisha pamoja haujapatikana miongoni mwa wanachama. ( hususan wakiihusisha Tanzania)
- BRICS ni wafadhili muhimu, wawekezaji na washirika wa kibiashara na pia ni chanzo cha usambazaji wa miradi kwa Tanzania. Tanzania pia inaitazama BRICS kama chemchem ya mifano ya kuigwa-k.m katika miradi mikubwa ya kilimo au katika kuinua ufanisi wa wakulima wadogo kiuzalishaji ambayo ndiyo sifa iliyofanikisha mapinduzi ya kijani ya India.
- Kutofanana miongoni mwa nchi wanachama wa BRICS imeleta hoja ya dhana ya manufaa ya pamoja. Licha ya uzingativu kuhusu uhalali na uwajibikaji, mjadala juu ya umasikini na kutokuwa na usawa ni wa msingi kwa ajili ya ubia wowote na BRICS ukizingatia kwamba umejikita katika ukuzaji wa uchumi na miundombinu (kwa mfano China). Shughuli za Miradi ya misaada na ile ya uwekezaji inayoongozwa na BRICS zimekuwa na

madhara makubwa sana kama vile matumizi mabaya ya maliasili, uporaji wa ardhi, kilimo na hifadhi ya chakula- sio kwa Tanzania tu, bali pia Amerika ya Kusini, Asia, na Ulaya Mashariki ambako wanachama wamekuwa na maslahi yakiuchumi na kisiasa.

- Kwa Tanzania, ambapo umaskini, utegemezi wa misaada, ukosefu wa chakula, miundombinu hafifu, kukosekana kwa uwezo wa uzalishaji na kuhamisha na kumudu gharama za teknolojia vimebakia kuwa changamoto, nafasi ya BRICS inaweza kuonekana kama fursa ya kuimarisha ushirika wa wanachama wa kundi la BRICS, ambao wanatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya Tanzania.
- Kwa namna nyingi wimbi la kuingia kwa BRICS katika eneo la Tanzania[82], huku wakiwa wameleta mijadala mbalimbali na mbinu zilizowafanikisha zilizojikita kwenye msingi wa uzoefu wa maendeleo yao ya hivi karibuni, imefungua fursa kwa mapambano ya kutafuta maendeleo na kuongeza mbinu za kupenya kwa Tanzania. Njia ya zamani yenye masharti finyu haitumiki tena, na Serikali ya Tanzania haihitaji tena kubanwa na masharti ya misaada ya Kimaendeleo ya nchi za magharibi. Wahusika tofauti tofauti wanaweza kufanya biashara kati ya wao kwa wao: kwa mfano wahisani wa maendeleo wa magharibi kwa ajili ya ustawi na usalama wa jamii, China kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu, India kwa ajili ya kubadilishana teknolojia ya kilimo na uendelezaji wa biashara ndogo ndogo na za kati. Hata hivyo, hakuna uhusiano unaokuja bila ya masharti. Licha ya dhana ya msingi inayosisimua ya ushirikiano wa nchi za kusini 'South South cooperation' ambao unalenga 'manufaa ya pande zote mbili'.
- China ndiyo yenye nguvu zaidi miongoni mwa BRICS na bila shaka ndiye mshirika aliyehodhi zaidi kama mbia na Tanzania. Baadhi yao wanaichukulia nafasi ya China katika ushirika huu kama mbia aliyehodhi kuwa ni neema, wakati wengine wanamtazama kama mshirika anayetafuta maslahi binafsi. China inatoa fursa ya ajabu kwa ajili ya majadiliano ya kibiashara kwa Tanzania. Fursa hii ya Majadiliano inasema: nchi yenu ina utajiri mwingi, lakini hamutumii kwa manufaa yenu. Mnaweza kudhibiti kile mlichonacho na kile tunachokihitaji ili kutumia rasilimali hizi kupata fedha za kujengea miundombinu ambayo mnaamini ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yenu. Vyovyote mtazamo wa China ulivyo, China haionekani kuwa na nia ya kurudi nyuma bali imedhamiria kuimarisha nafasi yake nchini Tanzania.
- Pamoja na kwamba Tanzania imekuwa ikisherehekea ubia wake na BRICS kama mbia mbadala wa biashara ya zamani na washirika wa nchi zilizoendelea za magharibi, utaratibu mzima wa kibiashara kati ya Tanzania na BRICS unaakisi ule kati ya Tanzania na nchi zilizoendelea zenye viwanda, huku Tanzania ikiwa ndiyo chanzo cha malighafi kwa nchi za BRICS na soko la nje la bidhaa zinazotengenezwa na BRICS. Kwa kuongezea, biashara

[82] Hii imetumika hapa sababu India na China sio wageni kibiashara Tanzania

kati ya baadhi ya nchi za BRICS na Tanzania inajumuisha ukwepaji wa kodi katika sekta ya misitu lakini pia inaaminika kutokea katika sekta ya wanyamapori na sekta nyingine. Zinaikosesha Tanzania kiasi kikubwa cha mapato yatokanayo na kodi.

- Tanzania ni moja kati ya nchi zinazonufaika na mbio za kuelekea uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs), kutoka nchi za BRICS ambazo ziko katika namna tofauti na vyanzo tofauti kutoka kwa wajasiriamali binafsi hadi mashirika ya uwekezaji ya umma. Wakati ambapo sekta za maliasili na miundombinu ndizo zinazotafutwa sana na BRICS katika uwekezaji, idadi ya miradi binafsi katika sekta nyingine inakua. Licha ya kuwa serikali ya Tanzania imekuwa ikitoa misamaha ya kodi kwa nia ya kuvutia na kuimarisha kiasi kikubwa cha wawekezeji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs) kuja nchini, kumeongezeka hofu kuwa kuendelea kutumia misamaha ya kodi kama njia ya kuvutia wawekezaji toka nchi za BRICS kunadhoofisha uwezo wa Tanzania katika kuongeza mapato ya kodi ambayo yangeiinua taifa hili kutoka katika umasikini na kuifanya ipunguze utegemezi wa misaada toka nje.
- Kukosekana kwa muundo ulio wazi kama mwongozo wa ushirika wa BRICS naTanzania, shinikizo la kimaadili na kisiasa halijafanyiwa kazi vya kutosha kwa kuwa sera za ushirika wa Tanzania na BRICS haziwiani na mikataba iliyopo ya kimataifa inayohusiana na misaada, biashara, uwekezaji, uhamiaji, umaskini, mambo ya utawala. Katika ngazi ya kitaifa Tanzania, (kwa kadiri tunavyofahamu) hakuna ushahidi wa nchi za BRICS kuwianisha utendaji kazi wao katika maeneo haya. BRICS pia haishirikiani kupitia 'makundi'yaliyorasimishwa ya washirika wa maendeleo Tanzania. Wanachama wa makundi haya mara nyingi wanawasiliana au kujadiliana baina ya nchi mbili au katika ngazi ya kimataifa kwa ajili ya biashara, uwekezaji, nk.
- Mkutano maalum wa kimataifa uliofanyika Busan (Busan High level Forum) unawakilisha makubaliano mapya zaidi duniani ambayo yanahimiza nchi nyingi zaidi kufuata kanuni zinazohusiana na muundo wenye ufanisi wa misaada ya kimataifa, hasa "wafadhili wanaoibuka". Changamoto imebakia katika kuunda mfumo ambao utawafanya wachama wote wasio wa DPG (yaani BRICS) kila moja binafsi anaweza kuunga mkono kanuni za msingi ya ajenda ya Tanzania kwa ajili ya ushirikiano wa maendeleo.
- Kadiri BRICS na Tanzania wanavyoendelea kuimarisha uhusiano, mifumo na uwezo wa miongozo, ufuatiliaji na tathimini na kuwajibika katika shughuli zake havijapewa kipaumbele na uwekezaji unaostahili ili kuhakikisha malengo yaliyotarajiwa yanatimia. Mara kwa mara kukosekana kwa uwazi na taarifa kutoka ushirikiano wan nchi za kusini (Southern Coorperation), masharti na vigezo vinavyohusiana na ushirika ambao unashusha ufuatiliaji na tathimini (M&E). Kwa mfano, kuwa na taarifa zenye kujitosheleza, kwa wakati na zenye ulinganifu unaostahili juu ya kiasi gani kimetumika katika

kufanya nini na nani anahusika katika sera za mipango, maamuzi na kujifunza. Kukosana kwa uwazi juu ya rasilimali za misaada inaleta ugumu katika kuona picha halisi na kuwa na uwezo wa kubadilisha uamuzi kuhusu maeneo ya "yatima" au "yanayopendeka" ambapo misaada inakuja bila uwiano kwenye sekta fulani, mkoa au wizara fulani hata pale mipango ya nchi nufaika inashauri vinginevyo. Tathimini ya mafanikio na kufikiwa matokeo makubwa ya maendeleo ya shughuli zilizofanyika ambazo ziinaashiria kundi la OECD-DAC, haijapata kupewa umuhimu unaostahili unaoelekeza kwamba kama ushirika wa nchi za kusini unapaswa unaolenga katika kujifunza na kubadlishana uzoefu, ufuatiliaji na tathmini ya uzoefu huu lazima ufanyike katika namna ya uwazi ili kuhakikisha kwamba watu wanajifunza mambo yaliyo sahihi.

## 7.0 HITIMISHO

BRICS ni wahisani muhimu, wawekezaji na washirika wa kibiashara na pia chanzo cha miradi ya ukandarasi kwa Tanzania. BRICS ikijipanua na kuzama zaidi katika ushirika na Tanzania inaipa nchi hii fursa kubwa ya kukua na mabadiliko ya uchumi. Kwa mfano, China na India hivi karibuni zimekua sana kiuchumi kiasi cha kuongeza uwepo kama wafadhili wa maendeleo nchi za nje (Oversease development aid (ODA), hali ambayo inaleta hofu na hamasa miongoni mwa wafadhili wa misaada waliojijenga.

Mwisho wa yote, itategemea na maono ya busara ya uongozi wa kitaifa na nguvu ya Taasisi za Kitanzania kushawishi ubia na BRICS uwe kwa ajili ya manufaa ya watu wa Tanzania. BRICS (na kwa maana hiyo nchi nyingine yoyote ya kigeni) havitaibadilisha Tanzania.

Ni Watanzania ndio watakaoibadilisha Tanzania! Ni kweli Kwamba misaada ya nje na jina jema vingekuwa na manufaa makubwa, lakini haviwezi kuchukua nafasi ya dhamira ya dhati ya watanzania wenyewe. Licha ya kuwa na kazi hii ya kupanda mlima, tunapendekeza yafuatayo:

1. Taarifa za wakati na uchambuzi wa kina wa ushirika wa BRICS na matokeo yake kwa Tanzania na chi nyingine za Afrika zina upungufu wa uwingi na ubora.wala hatufahamu kama mamlaka za BRICS zenyewe zinatathmini masuala hayo. Bila taarifa, wabunge na wananchi hawawezi kuwawajibisha viongozi wa serikali, hii ina maana rasilimali za umma haziwezi kusimamiwa ipasavyo wala kuwajibika nazo. Haya yanaweza kushugulikiwa kwa, (i) kuhimiza na kuwezesha ushirika kati ya watafiti na watunga sera kutoka Tanzania na wale wa nchi za BRICS. (ii) kuboresha wigo wa ufahamu wa wataalamu wa ngazi ya juu wa kitanzania juu ya sera za BRICS kwa kupanua kazi za pamoja za kitaaluma na wanataaluma wa BRICS, na (iii) kueleza wazi wazi kwamba sheria ya uhuru wa habari lazima itumike na kuzingatiwa ili kwamba umma wa watanzania uwe na haki ya kuhoji na

kutathimini taarifa juu ya makubaliano ya mikopo, biashara, na uwekezaji, na pia misaada ya wahisani wapya na wa zamani, kabla na baada ya makubaliano kutiwa saini.

2. Kuhusiana na hapo juu, nchi za BRICS zinahitaji kuwa makini na wazi-katika mazungumzo yao na Tanzania, na katika mfumo unaokubalika wa nchi zaidi ya mbili,-katika kuelezea jinsi inavyotaka kuchangia maendeleo ya Tanzania na kupunguza umasikini kama ilivyowekwa wazi katika mpango wa MKUKUTA. BRICS itahitajika kuweka wazi jinsi gani maono yake juu ya ushirika wa ushirika wan nchi za kusini utakavyoweza kuleta fursa bora kwa Tanzania na kupunguza umasikini. Ni vyema kwa serikali ya Tanzania kujiunga katika BRICS kwa kuzingatia sera zake za maendeleo, kuhakikisha kuwa misaada ina tija na inatoa mbadala, kuliko kushindana na wafadhili wa zamani. Ni muhimu pia kwa nchi za BRICS kuweka umakini kwenye matokeo ya misaada yake kwenye mambo ya utawala na juu ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs).
3. Ushirika wa BRICS umezidi kuwa na muhimu zaidi nchini Tanzania lakini uwepo wao haujaelezewa katika njia za midahalo. Kwa kuwa BRICS ina ofisi Tanzania, lazima washiriki katika ngazi ya kitaifa katika mijadala ya mwaka (Mfano DPG, GBS Review, Annual Poverty Policy week, makundi ya MKUKUTA na MKUZA n.k) au au kujihusisha kusiko rasmi na Mfumo wa Wafadhili wa maendeleo. Hili litawavuta karibu na mifumo na sera za taifa.
4. Hali ya BRICS kugombea maliasili nchini Tanzania inaweza kupelekea kuvunjwa kwa kanuni za utawala bora,(kama rushwa japo hakuna ushahidi katika hoja ya Tjønneland et al – 2006 kuhitimisha kwamba China ni wala rushwa kuliko nchi nyingine[83]). China na nchi nyingine zaidi zinazoibuka kwa ufahamu wetu wa sasa-hazijatoa msaada wa kutosha kuimarisha uwezo wa Taasisi na mamlaka za udhibiti nchini Tanzania. Hili linapingana kabisa na misaada kutoka nchi wafadhili wa zamani ambao wameyasisitiza masuala haya.
5. Sekta binafsi, ndiyo ambayo imechukua nafsi kubwa zaidi kuliko wizara za serikali, katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na ubadilishanaji kati ya uchumi na uchumi. Kuwasili kwa wajasiriamali na makampuni ya biashara kutoka katika nchi za BRICS kungeweza kuuhuisha uchumi wa Tanzania, lakini ili kufanya hivyo kunatakiwa sera stahiki, na uhimizaji wa uwekezaji kwenye viwanda sahihi. Tanzania haina budi kuendelea kutilia mkazo suala la kuajiri wafanya kazi wa Tanzania wenye utaalamu

[83] Tjonneland, Brandtzoeg, Kolas & le Pere: China ndani ya Afrika: Matokeo kwa Mipango ya maendeleo ya Norway. Wizara ya Mambo ya Nje ya Norway na Norad, 2006. www.cmi.no/publications/file/?2438=china-in-africa-implications-for-norwegian

[84] Serikali Inataka Kuzuia Makampuni ya China kutoa Huduma kwa Mradi wa Umeme wa Liganga-Mchuchuma ili Watanzania Waweze Kufaidika zaidi na Mradi huo. (Tarimo, 2012) ‵′Liganga-Mchuchuma Power Project to Benefit Tanzania′′ 17/05; The Guardian iliyopatikana kutoka: http://www.ippmedia.com/frontend/index.php?I=41643 (ilipatikana 17/05/2012)

kwa ajili ya miradi inayohudumiwa kwa fedha za kigeni[84] na kuhamasisha aina za uwekezaji unaohamisha utaalam, teknolojia na maarifa ambavyo vinaimarisha ushindani.

6. Idadi kubwa ya wahamiaji inayozidi kuongezeka kutoka nchi za BRICS wameamua kusafiri umbali mrefu kuelekea nchi mbalimbali za Afrika. Suala la uhamiaji linaonekana kugeuka kuwa donda ndugu (maumivu makubwa) kama halitashughulikwa kwa uzito unaostahili na serikali za Afrika zinazowapokea. Katika miaka ya karibuni, wananchi wa Afrika wameanza kukosa uvumilivu wanapoona kuona wageni wakinufaika zaidi kuliko wenyeji kutokana na fursa zinazofunguka kwa ajili ya mafanikio ya mtu binafsi. Wahamiaji wanaongeza chumvi kwenye kidonda pale ambapo wengi wao wanakiuka (wanavunja) sheria na kuonesha kiburi kwa wenyeji wao. Kwa hivyo, kuna haja ya balozi za nchi za BRICS zilizoko Tanzania kuongeza uelewa na ufahamu kwa raia wa nchi zao kujua mambo ya msingi ya maadili (yanayofaa na yasiyofaa) katika nchi inayokuwa mwenyeji wao.

7. Sambamba na hilo la hapo juu, kuna umuhimu wa serikali za nchi za BRICS kujua diaspora zao. Nchi zinazowafahamu diaspora wake, zina nafasi nzuri zaidi ya kuwatumia vizuri. Zoezi la kuwatambua diaspora wanachi husika kwa ajili ya uwekezaji makini nchini Tanzania kunaweza kukahusisha ukusanyaji wa taarifa kuhusu diaspora na usikilizaji makini wa kuelewa kile ambacho diaspora kinaweza kinaweza kuchangia, kile ambacho kina utayari wa kukitoa na kile ambacho wanakitarajia kutoka kwa serikali ya asili. Kwa jinsi hiyo ni muhimu kupokea utofauti uliopo wa ajenda za diaspora, matakwa na mikakati yake.

8. Kutokana na kukosekana kwa uwiano katika biashara kati ya nchi moja na nyingine, hali hii inahitaji kufanyiwa kazi kwa kuchukua hatua za kimkakati ili kuinua kiwango stahiki cha uuzaji wa bidhaa za Tanzania kwenda nchi za BRICS. Kwa mfano, njia muafaka ingelikuwa ni kufanya mashauriano ya mara kwa mara juu ya utekelezaji wa tume ya pamoja ya uchumi na biashara (Agosti 1985) kati ya china na Tanzania ambayo inapaswa kuweka viashiria vya mafanikio ya utekelezaji na pia inapaswa kuungwa mkono kwa hatua za kivitendo kwa ajili ya jitihada za pamoja katika kukuza yale maeneo mahususi ya uuzaji bidhaa nchi za nje.

9. Mwisho/kadhalika (hili linaendana kwa kiasi kikubwa na kipengele kilichowekewa 'bullet' hapo juu) taasisi za Tanzania zilizopewa dhamana ya kuratibu misaada, biashara na uwekezaji zinapaswa kutumia nguvu kubwa zaidi katika kukusanya taarifa/takwimu toshelevu katika yale maeneo husika juu ya uhusiano wao na nchi za BRICS. Mfano mzuri ni ule ambapo wizara ya fedha imetengeneza mwongozo unaoitwa AMP (Aid Management Platform (mwongozo wa usimamizi wa misaada) kwa ajili ya masuala ya misaada.

policy forum

S.L.P 38486
Dar es Salaam
Namba za Simu: +255 22 2780200 / +255 782 317434
Tovuti:www.policyforum.or.tz
Barua pepe:info@policyforum.or.tz